SportPesa
TZS. 710,494,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



## Mchimbaji mdogo auawa mgodi wa Tanzanite One

UKURASA 3



## Rashford : Tumpe heshima Solskjaer

UKURASA 23

Nipashe
Jumamosi Novemba 27, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580777
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



### KESI YA MBOWE

# Nyaraka ushahidi wa komandoo zapingwa kortini

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**WASHTAKIWA DAWA ZA KULEVYA WAACHIWA HURU**
VIUNGA vya Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, vilitawaliwa na vilio vya furaha kutoka kwa wanaodaiwa...

UKURASA WA 17
**KIRUSI KIPYA CORONA CHAIBUA HOFU**
SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limefanya mkutano maalum jana kujadili kuhusu aina mpya ya virusi vya...



Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda (kushoto), akipata maelezo kuhusu zao la mchikichi, akiwa katika ziara ya kikazi Uganda. **Habari Uk. 3. PICHA: WIZARA YA KILIMO**

## Ufumbuzi uhaba wa mafuta ya kula nchini wapatikana

UKURASA 3

## ACT- Wazalendo yakoleza moto waliopata ujauzito kurudi shuleni

• **HakiElimu** nayo yaunga mkono uamuzi wa serikali... *Uk. 2*

**MICHEZO** **YANGA YAIHOFIA MBEYA KWANZA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Jamhuri yapinga nyaraka za komandoo kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MAWAKILI wa Jamhuri wameiomba Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kukubali mapingamizi waliyowasilisha kupinga kupokewa nyaraka ya upande wa utetezi kwa madai shahidi ameshindwa kujenga msingi na hakuna mtiririko.

Hoja za pingamizi ziliwasilishwa jana kwenye kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu, mbele ya Jaji Joachim Tiganga baada ya shahidi ambaye ni mshtakiwa wa tatu, Mohammed Ling'wenya, ambaye alijitambulisha kuwa ni komandoo, kuomba kutoa barua aliyopeleka kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Ilala kama kielelezo mahakamani.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavula alidai chanzo cha nyaraka sio shahidi aliyekuwa kizimbani.

Anadai shahidi ameshindwa kutengeneza msingi, akiomba barua hiyo isipokewe kwa kuwa shahidi hafai kuiwasilisha.

Akichangia hoja, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, alidai anaunga mkono hoja zote zilizowasilishwa na Wakili Chavula na kuongeza kwamba jina pekee la mshtakiwa halitoshi kufanya kielelezo hicho kipokewe, hakuna mahali shahidi alisema barua hiyo ilikuwa wapi na hajui kilichomo ndani.

"Shahidi hakueleza barua imefikaje kwake, hakuna sehemu iliyoonyesha barua hiyo kama ilipitia kwa askari magereza.

"Mawasiliano yaliyofanyika yalitakiwa kufanywa kupitia ofisa wa magereza. Tunaomba mahakama isipokee nyaraka hizo, ikubaliane na pingamizi letu, shahidi yuko chini ya magereza lakini ushahidi wake umepatikana kinyemela," alidai Wakili Hillar.

Akijibu hoja, Wakili Peter Kibatala alidai anaunga mkono hoja na anaomba barua ipokewe kama kielelezo.

Wakili Dickson Matata alidai hoja za Jamhuri hazina mashiko, hazina msingi na nguvu ya kisheria kusimama.

"Uhusiano wa wakili na mteja unalindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Ibara ya 13(6b) ya mwaka 1977 kama inavyofanyiwa marekebisho mara kwa mara.

Alidai barua ina majina ya shahidi, sahihi, kuna namba ya kesi na kuna jina la kiongozi wa jopo Wakili Peter Kibatala.

Barua hiyo ilikuwa inaenda kwa Kamanda wa Polisi Ilala, mshtakiwa alikuwa akiomba kupata baadhi ya taarifa.

## Vitambulisho vya NIDA vyadoda kwenye ofisi

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema hadi sasa vitambulisho 1,103,822 kati ya vile vilivyozalishwa na kusambazwa sehemu mbalimbali wilayani, bado havijachukuliwa na wanachi.

Aidha, kutokana na hali hiyo ameiagiza Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kutumia vyombo vya habari kutangaza majina ya watu ambao bado hawajachukua vitambulisho vyao.

Simbachawene alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya wizara hiyo kwa waandishi wa habari katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika.

Alisema miongoni mwa vitambulisho hivyo, 206,959 viko katika ofisi za usajili za wilaya na 896,863 viko katika ofisi za serikali za kata, vijiji, mitaa katika mikoa 31 Tanzania Bara na Visiwani.

"Kupitia fursa hii, nitoe maagizo kwa NIDA kuwa watumie vyombo vya habari yakiwamo magazeti kutoka majina ya watu ambao vitambulisho vyao vipo tayari na vipo katika maeneo gani ili waende kuvichukua ili kuondoa malalamiko yaliyopo hivi sasa," alisema.

Pia alisema mamlaka imefanikiwa kujenga na kutunza daftari la kielekroniki la usajili na utambuzi wa watu.

"Daftari hili kwa sasa lina namba za utambulisho 19,102,234 zilizounganishwa na alama za vidole. Namba hizi zinatumiwa na taasisi zingine katika kuhakiki taarifa za mwananchi kabla ya kumpa huduma," alisema Simbachawene.

Alisema baada ya kujenga kanzidata ya watu wote nchini kwa kutumia NIN, mamlaka imehamasisha matumizi ya namba za utambulisho wa taifa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

"Hivyo kwa sasa taasisi zinatumia kanzidata ya Mamlaka ya matumizi mbalimbali," alisema Waziri Simbachawene.



Meneja Uhusiano wa kampuni ya IPP, Nancy Mwanyika, akiongoza wafanyakazi wenzake kuchangia damu, katika zoezi lililofanywa na Kitengo cha Damu Salama cha Hospitali ya Taifa Muhimbili, kwenye viwanja vya ITV, Mikocheni Dar es Salaam jana. PICHA: SABATO KASIKA

# ACT yapongeza uamuzi wa serikali waliopata ujauzito kurejea shuleni

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimepongeza hatua ya serikali ya kukubali kurejeshwa shuleni na kuendelea na masomo kwa wanafunzi wanaopata ujauzito wakiwa katika shule za msingi na sekondari.

Mapema wiki hii, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, akitoa taarifa ya mafanikio ya sekta ya elimu kuelekea miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika, alisema serikali itaondoa vikwazo mbalimbali katika upatikanaji wa fursa za elimu.

Kwa mujibu wa Ndalichako, vikwazo hivyo ni pamoja na kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo yao kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kupata ujauzito. Taarifa iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Ngome ya Wanawake ya ACT- Wazalendo, ilisema hatua hiyo ni ya msingi katika utekelezaji wa haki za watoto pamoja na mikataba ya kimataifa kuhusu watoto.

Alisema suala hilo limo katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 ya chama hicho, hivyo wanaunga mkono uamuzi huo ingawa serikali ya awamu ya tano ilipinga na kufuta jambo hilo kwa wanafunzi wanaokumbwa na matatizo hayo kurudi shuleni na kupata elimu katika mfumo rasmi. "Hatua hii ilifikiwa kwa matamko ya hadharani yaliyotolewa na viongozi wa serikali wakiongozwa na Rais mwenyewe, Hayati John Pombe Magufuli kwa madai kwamba serikali yake haiwezi kusomesha 'wazazi'.

"Chama chetu, kupitia kwa Kiongozi Mkuu Zitto Kabwe, kilichukua msimamo na hatua kali dhidi ya uamuzi ule wa serikali ya kuwanyima watoto elimu kwa sababu ya ujauzito. Wadau wengine pia walijitokeza na kupaza sauti zao na kupingana na uamuzi wa Rais Magufuli na serikali yake," ilisema taarifa hiyo.

Hatua hiyo ya Zitto ilisababisha kushambuliwa kukashfiwa na kuitwa msaliti na baadhi ya viongozi wa serikali na ndani ya Bunge na wabunge wa CCM.

Kukashfiwa huko kwa Zitto, taarifa hiyo ilisema, ilitokana na uamuzi aliochukua wa kuishawishi Bodi ya Benki ya Dunia (WB) kutoipa serikali ya Rais Magufuli mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 500 (sawa na zaidi ya Sh. trilioni 1.1 za Kitanzanai) uliolenga kuboresha mfumo na miundombinu ya elimu.

Zitto aliikumbusha Bodi ya Benki ya Dunia inayotoa idhini kutolewa kwa mkopo huo kuwa mkopo huo utakuja kutumika kwa ubaguzi kwa kuwaacha nje watoto wengine kwa kisingizio kuwa wamepata ujauzito wangali shuleni na hivyo hautaweza kufikia lengo lililokusudiwa la kuwakomboa watoto wa Kitanzania kielimu.

**HAKI ELIMU YANENA**

Taasisi ya HakiElimu imeipongeza serikali kwa kuruhusu wanafunzi waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito kurudi shuleni. Hata hivyo, imeishauri serikali kukazia waraka huo mpya unaowaruhusu kurejea shuleni, kufanyia mabadiliko sera na sheria ya elimu ili iwe rasmi badala ya kuishia hivyo ulivyotolewa.

Taasisi hiyo pia imeiomba serikali kuandaa mwongozo ambao utaeleza bayana namna mwanafunzi anayepata ujauzito akiwa shuleni, anavyoandaliwa kisaikolojia wakati anaondolewa kurudishwa nyumbani kwenda kujifungua na hatua anazotakiwa kufuata wakati anarejea tena baada ya kujifungua.

"Na mwongozo huo ndio utaeleza mambo mengi kwa uwazi, baada ya kujifungua arudishwe kwenye shule ile ya awali au vinginevyo, nani atahusika wakati wa kumpokea wakati anarejea na taratibu nyinginezo,"alisema Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kallaghe.

"Lakini pia waraka huu ukitumika na ikatamkwa rasmi kwenye sera na sheria inakuwa ndio uhakika na si rahisi hata kiongozi mwingine anapoingia kubadilisha kuliko ikibaki kwenye waraka tu kama hivyo ulivyotolewa," aliongeza.

Dk. Kallaghe alisema uko mwongozo ambao serikali iliwahi kuuandaa mwaka 2009 ambao ulikuwa ukieleza namna wanafunzi hurejea shuleni baada ya kukatiza masomo yao, lakini haukuwahi kutumika wala kutiwa saini na kushauri kwamba endapo serikali itaridhia inaweza kuutumia kwa sasa.

Dk. Kallaghe alisema takwimu za Elimu (BEST 2020) mwaka 2015 zinaonyesha kuwa wanafunzi wa kike 3,439 waliacha shule kwa sababu za ujauzito na idadi iliongezeka hadi kufikia wanafunzi 6,533 mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la asilimia 90.

HABARI KITAIFA

# Mchimbaji auawa mgodi wa tanzanite

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MCHIMBAJI mdogo wa madini ya tanzanite, Faraja Metili (40), mkazi wa Ilkiding'a wilayani Arumeru mkoani Arusha, anadaiwa kuuawa na walinzi wa mgodi wa Tanzanite One, huku wenzake wanne wakishikiliwa na polisi baada ya kukutwa katika mgodi huo uliosimamishwa uzalishaji na serikali.

Akizungumza jana na Nipashe, kaka wa marehemu, Karimu Elias, alisema ndugu yao baada ya kufariki dunia na mwili wake kufanyiwa uchunguzi katika Hospital ya Mount Meru, ilibainika chanzo cha kifo chake ni kipigo.

"Mdogo wangu amefariki dunia kwa kipigo alichokipata toka kwa baadhi ya walinzi wa mgodi huo baada ya kumtuhumu kuingia katika mgodi kinyume cha utaratibu," alilalamika.

Alisema kitendo cha kumpiga na kusababisha kifo ni ukiukwaji wa sheria kwa kuwa hata kama mdogo wake alikuwa na makosa, haihalalishi kumuua.

Alisema ingependeza kumkamata na kumpeleka kwenye vyombo vya sheria kama wenzake aliokuwa nao ambao wanashikiliwa na polisi mkoani humo.

"Tunajipanga kwenda mahakamani kulalamikia kitendo hicho na tunaomba serikali iingilie kati na wahusika wachukuliwe hatua," alisema.

Ndugu huyo alitishia kuwa serikali isipochukua hatua, ndugu watafanya alichokiita 'kuvunja chungu' ili wahusika wa tukio hilo 'yawakute mmoja baada ya mwingine'.

Kaka mwingine wa marehemu, John Silasi pamoja na mjomba wa marehemu, Samweli Ngalabale, walisema wanasikitishwa na kifo cha ndugu yao na kuomba hatua zaidi kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

Walisema ndugu yao ameacha watoto wawili na mjane na baada ya kufanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Rufani Mount Meru mkoani Arusha, ndugu walikabidhiwa mwili huo na waliuzika juzi katika Kijiji cha Ilkiding'a wilayani Arumeru.

Kamanda wa Polisi mkoani Manyara, Harrison Mwakyoma, alithibitisha tukio hilo na kueleza kwamba Jeshi la Polisi linawashikilia watu wanne wanaodaiwa kuingia kinyume cha sheria katika mgodi wa Tanzanite One ambao serikali imesimamisha uzalishaji na watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

"Suala la marehemu kuuawa na walinzi mimi silifahamu ila polisi wanafanya uchunguzi juu ya tukio hilo," alisema Mwakyoma.

Wakati huo huo, mfugaji anayejulikana kwa jina Lobisingi Kairo (15), mkazi wa Kijiji cha Olorien Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, anadaiwa kuuawa kwa kuchomwa mkuki mgongoni na kijana mwenzake mwenye umri wa miaka 13.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alisema kuwa tukio hilo lilitokea Novemba 24, mwaka huu, majira ya saa mbili asubuhi baada ya kutokea mzozo wakati wakichunga mifugo.

Alisema kuwa baada ya tukio hilo, kijana huyo alikimbizwa katika zahanati iliyopo katika kijiji hicho kwa lengo la kuokoa maisha yake lakini baada ya kufika katika zahanati hiyo waligundua alikuwa ameshafariki dunia.

Masejo alisema Jeshi la Polisi linamsaka mtuhumiwa huyo ambaye jina lake linahifadhiwa baada ya kukimbia alipofanya unyama huo.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia), akiteta jambo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, wakati wa mkutano wa majadiliano ya kimkakati kati ya Serikali na washirika wa maendeleo uliowahusisha Mawaziri, Mabalozi, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia, jijini Dar es Salaam. **PICHA: WFM**

# Uhaba wa mafuta ya kula watafutiwa dawa

**Na Mwandishi Wetu, KAMPALA**

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amezuru kikazi Uganda na kufanya mazungumzo na Waziri wa Kilimo, Mifugo, Viwanda na Uvuvi, Frank Tumwebaze pamoja na timu ya wataalamu kutoka Tanzania na Uganda.

Katika ziara hiyo, Waziri Mkenda ameambatana na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Kamishna wa Polisi Thobias Andengenye na wataalamu wa kilimo kutoka Wizara ya Kilimo na Mkoa wa Kigoma.

Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa mikoa ya kimkakati katika uzalishaji wa zao la mchikichi nchini.

Ziara hiyo imelenga kuimarisha uhusiano wa Uganda na Tanzania katika sekta ya kilimo ili kukuza tija ya uzalishaji wa mazao kwa kutumia mbinu bora za kilimo, ikiwa ni pamoja na kuimarisha utafiti wa kilimo na upatikanaji wa mbegu bora.

Katika mazungumzo yao hayo juzi, Waziri Mkenda alieleza jitihada zinazofanywa na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan za kukuza uchumi kwa kuimarisha uhusiano na chanya na nchi jirani kama Uganda.

"Tumekuja Uganda kwa kuwa tunafahamu sisi ni ndugu na uhusiano wetu una historia ndefu. Marais wetu wote wawili, Rais Yoweli Museven na Rais Samia Suluhu Hassan wanafanya kazi nzuri ya kuimarisha uhusiano uliopo na kukuza uchumi wa nchi zote mbili," alisema.

Waziri Mkenda alisisitizia Wizara ya Kilimo ipo katika mkakati kabambe wa kuhakikisha nchi inaondokana na dosari ya uhaba wa mafuta ya kula na kutumia fursa ya ziara hiyo kujifunza namna ambavyo Uganda imepiga hatua kubwa ya kilimo cha michikichi.

Alisema hatua hiyo itaongeza hamasa kwa uwekezaji mkubwa wa kilimo hicho nchini na kulimwa kwa tija na kupunguza uhaba wa mafuta ya kula kwa kiwango kikubwa na kushusha bei kwa mtumiaji.

"Katika ziara hii nimeongozana na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Kamishna wa Polisi Thobias Andengenye kwa kuwa Kigoma ni mkoa mmojawapo wa kimkakati kwa kilimo cha michikichi.

"Kuja kwake huku kutawezesha kujionea na kujifunza ili kwenda kuwahamasisha wakulima wetu kulima kwa tija," Prof. Mkenda alisema.

Ziara hiyo pia ilihusisha kutembelea mashamba makubwa ya mchikichi, viwanda vya uchakataji wa mafuta ya mawese na kujifunza mfumo mzima wa ulimaji na utunzaji wa mchikichi na hadi kupata mafuta ya mawese.

Kampuni ya Wilmer yenye matawi katika nchi zaidi ya 25, ina nia ya kuongeza uzalishaji Tanzania katika kuzalisha mafuta yatokanayo na michikichi, alizeti na mazao mengine.

Kampuni hiyo imejenga kiwanda cha mchele mjini Morogoro chenye uwezo wa kukoboa mpunga tani 200 kwa siku, kilichofunguliwa rasmi na aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Pombe Magufuli mapema mwaka huu.

Waziri wa kilimo, Mifugo, Viwanda na Uvuvi wa Uganda, Tumwebaze, alimshukuru Waziri Mkenda na timu yake kwa kuamua kutembelea Uganda na kuonyesha undugu na urafiki wa nchi hizo mbili.

Aliongeza kuwa Uganda iko tayari kuendelea kuimarisha uhusiano na Tanzania katika sekta ya kilimo na kutaka wataalamu wa kilimo wa nchi zote mbili kuharakisha uundwaji kamati ya pamoja ya kilimo ili kutekeleza makubaliano ya ushirikiano wa pamoja katika kilimo yaliyotiwa saini Septemba 6, 2019 jijini Dar es Salaam.

"Tumekubaliana nchi zetu kushirikiana katika mambo mbalimbali kwenye sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa mbegu bora, masoko, utafiti na mengineyo.

"Tumefurahi sana kwa ujio huu wa Waziri wa Kilimo wa Tanzania kwa kuwa ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano hayo," alisema Waziri Tumwebaze.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Wilmar anayesimamia Afrika, Santhosh Pilai, alisema kampuni hiyo iko tayari kuongeza uwekezaji mkubwa zaidi Tanzania ili kumhakikishia mkulima soko pamoja na kuondoa vikwazo vya uhaba wa mafuta ya kula Tanzania.

"Tumefanya uwekezaji katika nchi zaidi ya 20 Afrika, Asia na Marekani na kwa Tanzania tuwekeza kiwanda kikubwa pale Morogoro na tunataka kuwekeza zaidi Tanzania. Zaidi ya vijana 400 wameajiriwa katika uwekezaji huo," alisema Pilai.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
26 – 11 - 2021

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe **27 – 11 – 2021** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Dar es salaam Port kuelekea Rufiji, gari zenye namba za usajili:

**T 133 CCP /T 139 CHN, T 135 CCP /T 837 CHK**
**T 905 DSD /T 969 CPS, T 896 DSD /T 974 CPS**
**T 305 CZS /T 310 DDH, T 156 BTE /T 385 DHQ**
**T 649 BZU /T 416 AYQ, T 403 DFE /T 387 DQH**
**T 217 BYM /T 777 AQR, T 528 BKC /T 393 DVS**
**T 515 BKC /T 394 DVS, T 210 BYM /T 137 CHN**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 23.00 |
| Upana | - | mita | 4.40 |
| Kimo | - | mita | 5.20 |

3. Njia itakayotumika: Dar es salaam , Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

216590302

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# NHC yapewa mchongo uwekezaji mji Kahama

**Na Munir Shemweta, KAHAMA**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limetakiwa kufanya uwekezaji wa majengo ya biashara na nyumba za kupangisha katika mji wa Kahama kutokana na mji huo kuendelea kukua kwa kasi.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk Angeline Mabula, alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara yake ya siku mbili mkoani Shinyanga kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na miradi inayosimamiwa na NHC.

Alisema Kahama ni mji unaokua kwa kasi kubwa na kama NHC haijafikiria kuwekeza katika mji huo, ijipange kuona namna gani inaweza kutumia fursa ya kukua huko kwa mji kwa kufanya uwekezaji na kusisitiza kuwa hata kama hakuna uhitaji wa nyumba za kuuza, shirika linaweza kujenga majengo ya biashra yanayoweza kupangishwa.

"Uwekezaji wowote mtakaoufanya hapa Kahama kama hakuna walioonyesha dhamira ya dhati ya kununua basi jengeni nyumba za kupanga ili kuwa na nyumba za kutosha mji unakuwa haraka," alisema Dk. Mabula.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, kila mahali ambapo NHC imewekeza katika majengo ya kibiashara hakuna sehemu imekosa wapangaji na kadri mji wa Kahama unavyokua kwa kasi, bado NHC inaweza kufaidika.

Alimwagiza Meneja wa NHC Mmkoa wa Shinyanga kufanya uamuzi ya haraka kwa lile eneo lililoainishwa na Manispaa ya Kahama kwa kwa ajili ya uwekezaji na kusisitiza kuwa Kahama bado inazo fursa nyingi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama ambaye ni Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili, Clemence Nkusa, alimwambia Naibu Waziri kuwa tayari halmashauri yake ilishatenga eneo kwa ajili ya shirika hilo kufanya uwekezaji.

Kutokana na hatua hiyo, Naibu Waziri Mabula aliitaka NHC kufanya uamuzi wa haraka na kufikia Desemba, mwaka huu, wizara iwe imepata taarifa ya aina ya uwekezaji utakaofanyika.

Dk. Mabula pia aliitaka NHC kufikiria namna ya kufanya uwekezaji wa nyumba katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kutokana na kuwa na uhitaji wa nyumba, zikiwamo za watumishi.

# Wabunge waitaka serikali kujali wachimbaji madini

**Na Gerald Kitabu**

WABUNGE wameishauri serikali kujali maeneo ambayo yanachimbwa madini kwa kuboresha huduma za jamii.

Katika mkutano wa siku moja ulioandaliwa na shirika la Friedrich Ebert Stftung (FES) kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama Vinavyotoa huduma kwa umma duniani (PSI), watunga sheria hao walisema maeneo mengi ambayo yanachimbwa madini, wakazi wake wana maisha duni, ikiwamo kukosekana kwa huduma muhimu za jamii.

Mkutano huo ulijikita katika kutoa ushauri wa kisera kwa wabunge na serikali uliotokana na utafiti uliofanywa na watalaamu wa masuala ya kodi kutoka katika mashirika hayo pamoja na shirika la Actionaid.

Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko (CHADEMA), alisema serikali inapaswa kurekebisha utaratibu wa sasa wa kukusanya mapato kutoka katika maeneo ya machimbo na kupeleka serikali kuu badala yake warudishe kiasi fulani kuboresha huduma za jamii mahali ambapo madini hayo yanachimbwa.

Akitolea mfano Tarime, mbunge huyo ambaye yupo katika Kamati ya Bajeti ya Bunge, alisema wilaya hiyo ina maeneo yanayochimbwa dhahabu lakini kampuni zinazochimba madini hayo hazijafanya jitihada zozote za kuiendeleza wilaya hiyo ikiwamo kuboresha maisha ya wananchi wanaozunguka eneo la mgodi.

"Uzoefu unaonyesha kuwa wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka maeneo ya migodi wana maisha duni na wengi hawana maji, barabara nzuri, huduma za afya na shule.

"Nashauri serikali kuweka sera itakayozifanya kampuni za madini kuboresha maisha ya watu kupitia mirahaba na mapato yatokanayo na kodi katika maeneo ya uchimbaji wa madini," alisema.

Mbunge wa Geita, Constantine Kanyasu (CCM), alisema serikali inatakiwa kuja na sera itakayofanya madini yawe na manufaa kwa wananchi wa hali ya chini.

"Nashauri tubadilishe sera yetu ili madini yanufaishe maisha ya wananchi na sisi kama wabunge tuna kazi ya kufanya ili kuwezesha suala hili," alisema.

Pia alishauri serikali kutafuta njia za kukabiliana na utakatishaji wa fedha ikiwamo kuimarisha na kutekeleza sheria ili kupambana na hali hiyo kwa kuwa ni biashara inayohusisha watu wenye utalaamu.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, Nusrat Hanje, alisema kama serikali ingezibana ipasavyo kampuni za uchimbaji wa madini isingekuwa inasumbuka kufuatilia kodi ndogo kwa wananchi wa kima cha chini.

"Hivi karibuni serikali iltangaza kukusanya kodi kupitia simu za mkononi. Hili lingemalizwa na kodi kutoka katika kampuni za madini.

"Serikali inabidi izibe mianya ya ukwepaji kodi ili ipate fedha za kutosha kuboresha maisha ya wananchi wa kima cha chini," alisema.

Akielezea lengo la mkutano huo, Ofisa Mradi kutoka Shirika la Friedrich Ebert Stiftung (FES) Tanzania, Anna Mbise, alisema ni kutoa ushauri wa kisera uliotokana na utafiti uliofanywa na watalaam wa maswala ya kodi uliofanyika na mashirika ya FES na PSI mwaka 2018 na Actionaid Tanzania mwaka 2021 kwa wabunge wa kamati mbalimbali za Bunge la Tanzania.

Madhumuni ya utafiti huo ilikuwa kutafiti njia mbalimbali ambazo serikali imekuwa ikipoteza mapato na kutoa ushauri wa njia bora za kukabiliana na hali hiyo ili kuongeza mapato kwa ajili ya kuboresha maisha ya wanachi wa hasa vijijini.

Mashirika ya FES, PSI na Actionaid yalifanya utafiti ambao ulionyesha kuwa serikali inapoteza mapato mengi kutokana na ukwepaji wa kodi, misamaha ya kodi na mianya mingine kutoka kwa kampuni mbalimbali.

"Tumetoa ushauri wetu kwa wabunge ya nini kifanyike, serikali inatakiwa kufanya nini ili kuongeza ukusanyaji wa mapato," alisema.

Shirika la FES, vyama vya wafanyakazi kutoka katika sekta binafsi, Actionaid, watalaamu na wadau wa kodi kutoka katika Asasi za kiraia tunaamini kuwa huduma bora za jamii zinawezekana iwapo kutakuwepo na utashi wa kisiasa wa kukusanya mapato yatokanayo na kodi kutoka katka sekta ya uziduaji.

Awali akiwasilisha mada, mshauri wa kodi kutoka shirika la Actionaid, Dk. Balozi Morwa alisema uwekezaji wa kampuni za uziduaji umekuwa na vikwazo vingi ikiwamo ukwepaji kodi na ukosefu wa uwazi katika mikataba yao.

Hivyo, serikali inapaswa kuimarisha sera zake ili kuhakikisha mapato yatokanayo na sekta hii yananufaisha wananchi na hata kugharamia mipango ya SDG's na kuinua uchumi wa nchi kwa ujumla.

Alisema kuwa katika nchi nyingi za Afrika zenye madini, sekta ya uziduaji haijanufaisha nchi husika.




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel (katikati), akikata utepe kuzindua duka la Vodashop, jijini Mwanza juzi. Ufunguzi wa duka hilo ni mwendelezo wa kampuni ya Vodacom Tanzania, kupeleka huduma zake karibu na wateja. Wengine ni Mkurugenzi wa Biashara wa kampuni hiyo, Linda Riwa (wa pili kulia) Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Hassan Masala (wa pili kushoto) na (kulia) ni Mkuu za Mauzo wa Vodacom Kanda ya Ziwa, Ayubu Kalufya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Washtakiwa dawa za kulevya waachiwa huru

**Na Hellen Mwango**

VIUNGA vya Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, vilitawaliwa na vilio vya furaha kutoka kwa wanaodaiwa kuwa ndugu na wanafamilia wa watuhumiwa tisa akiwamo Mwanaidi Mfundo waliokuwa wakikabiliwa na kesi ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya cocaine kilo tano, kuachiwa huru baada ya kukaa mahabusu miaka 10 na miezi mitano.

Kadhalika, mahakama hiyo imeamuru mali zote zilizoshikiliwa kutoka kwa washtakiwa warejeshewe na upande ambao haujaridhika ukate rufani.

Hukumu hiyo ilisomwa jana katika mahakama hiyo na Jaji Isaya Arufani, aliyekuwa akisikiliza kesi hiyo.

Jaji alisema mahakama yake bila kuacha shaka imepitia ushahidi wa mashahidi wanane wa Jamhuri na tisa wa utetezi, lakini hakuna ushahidi uliothibitisha makosa dhidi ya washtakiwa.

Alisema jukumu la kuthibitisha kesi mahakamani ni la Jamhuri lakini wameshinda kuthibitisha kesi hiyo, hivyo mahakama inawaachia huru.

"Mahakama hii inawaachia huru. Mali zote zinazoshikiliwa na Jamhuri zikiwamo nyaraka na hati za kusafiria zirejeshwe kwa washtakiwa na haki ya kukata rufani kwa upande ambao haujaridhika iko wazi," alisema Jaji Arufani. Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Monica Mbogo akisaidiana na Anastazia Wilson huku upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Richard Rweyongeza, Jacqueline Rweyongeza, Hajra Mungura na Domonic Nkwera.

Mbali na Mfundo (58), washtakiwa wengine ni raia wa Kenya, Anthony Karanja (42) na Ben Ngare, Sara Munuo, Almas Said, Yahaya Ibrahim, Aisha Kungwi na Rajabu Mzombe.

Juni 3, 2011 walisomewa mashtaka yao kwa mara ya kwanza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Waliposomewa mashtaka hawakutakiwa kujibu chochote na walikuwa mahabusu mpaka jana walipoachiwa huru baada ya kukosekana ushahidi.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa, Juni Mosi, 2011, eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikamatwa wakiingiza dawa za kulevya aina ya Cocaine. Washtakiwa walikana mashtaka hayo.

**HABARI KITAIFA**

## Mgogoro wa shamba wapatiwa ufumbuzi

**Na Joseph Mwendapole**

MGOGORO wa shamba lenye ukubwa wa ekari 302, maarufu kama kwa mkorea, Kigamboni jijini Dar es Salaam, uliodumu kwa miaka 17, umefikia tamati.

Hatua hiyo ilitangazwa jana na Meya wa Manispaa ya Wilaya ya Kigamboni, Ernest Mafimbo, alipozungumza na waandishi wa habari jana baada ya kikao cha Maalum Baraza la Madiwani.

Meya huyo alisema mgogoro wa eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 302 ulianza mwaka 2004 na umedumu kwa muda mrefu kutokana na mvutano uliokuwapo baina ya wananchi na mwekezaji.

Alisema kuwa baada ya vuta nikuvute ya miaka yote hiyo, sasa imekubaliwa mwekezaji huyo abaki na ekari 150 na wananchi wapewe ekari 152.

Alisema mgogoro huo wa muda mrefu umepitia hatua mbalimbali za utatuzi kuanzia wilaya, mkoa na Mahakama Kuu lakini hakukuwa na ufumbuzi wowote.

"Ilipofika wizara, yenyewe ilileta maelekezo kuitaka Manispaa ya Kigamboni kwamba baada ya kutoa tamko lake kuwa kiwanja cha wakorea mission ekari 302 eneo ambalo kwa asili lilikuwa linagombaniwa na wananchi na mwekezaji.

"Wizara ikaamuru wananchi wabaki na ekari 152 na mwekezaji huyo abaki na ekari 150. Manispaa ilipewa jukumu la kusimamia kuhakikisha hili linafanikiwa bila kuwa na tatizo lolote," alisema.

Aliongeza kuwa wananchi hao walishauri atafutwe mtu binafsi ambaye wanamwamini kwa ajili ya kupima viwanja hivyo na manispaa iwe kati ili mwisho wa siku mtaalamu huyo apime viwanja vyao.

"Mawazo yao tuliyapitisha kwa sababu lengo letu kubwa ilikuwa kuwaondolea kero wananchi hatukuwa na maslahi binafsi, hivyo tulikubali matakwa yao kwa sababu wao waliona tukifanya hivyo watapata haki," alisema.

Alibainisha kuwa mtaalamu huyo anaitwa Gombo Samandito ambaye amefanya mchakato wa kuchonga barabara, michoro iliyotoka kwenye viwanja hivyo kuweka mawe na kuhakikisha eneo zima limepimwa.

"Kwa hatua hii, sisi Baraza la Madiwani tutafuatilia kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa kuhakikisha wananchi wote wanapata haki zao na hakutakuwa na malalamiko tena," alisema.

Mmoja wananchi wanaotarajiwa kunufaika na viwanja hivyo, Mwajuma Omari aliishukuru serikali kwa kuhakikisha mgogoro huo wa muda mrefu unafikia tamati.

Maua Omari, mnufaika wa eneo hilo, alisema mwekezaji huyo mwaka 2006 waliwapa fedha kidogo kiujanja kwa lengo la kutwaa eneo hilo lakini baadaye wananchi waligoma kuondoka.

"Mwekezaji alipokuja mwaka ule hakuwa na utaratibu mzuri wa kuwalipa wananchi yeye alikuwa anakuangalia akiona mzee sana anaweza kukupa hata Sh 50,000, sasa mimi nilikuwa na ekari 1.5 lakini alinipa Sh. 100,000, ndiyo sababu wananchi wakaamka na kuanza kudai haki yao," alisema.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza na mmoja wa wafanyabiashara katika kituo cha mabasi mjini Kahama wakati wa ziara yake ya kukagua shughuli za sekta ya ardhi. **PICHA: WANMM.**

# Serikali kuimarisha afya za Watanzania

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema serikali imedhamiria kulinda na kuimarisha afya za Watanzania hasa wakati huu wa kuelekea kutimiza dira ya kuutokomeza UKIMWI nchini ifikapo mwaka 2030.

Alitoa kauli hiyo jana alipofungua Kongamano la Kisayansi la Kitaifa Kuhusu VVU na UKIMWI katika Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani kwenye Ukumbi wa Hoteli ya Mbeya Modern Highland jijini Mbeya.

Kaulimbiu ya kongamano hilo inasema "Zingatia Usawa, Tokomeza UKIMWI, Tokomeza Magonjwa ya Mlipuko".

Majaliwa alisema kaulimbiu ya kongamano hilo inaakisi dhamira ya serikali ya kulinda na kuimarisha afya za Watanzania hasa wakati huu wa kuelekea kutimiza dira ya kuutokomeza UKIMWI nchini ifikapo mwaka 2030.

"Hivyo basi, nitoe rai kwa jamii kutafakari upya nafasi waliyonayo na kupinga kwa nguvu zote masuala yote na tabia zinazochangia maambukizi mapya ikiwamo unyanyapaa, ukatili wa kijinsia, mila zinazochangia maambukizi, ngono katika umri mdogo, kuporomoka kwa maadili na tabia nyinginezo hatarishi.

"Kaulimbiu hii imekuja wakati mwafaka ambapo kama taifa tunahitaji kuihamasisha jamii na mtu mmoja mmoja kuzingatia usawa na kutoa mchango wake katika kufikia azma ya kutokomeza maambukizi mapya ya VVU hasa kwa vijana wetu ambao kwa mujibu wa takwimu wanachangia kiwango kikubwa cha maambukizi mapya," alisema.

Majaliwa alisema serikali itaendelea kuhamasisha wananchi na wadau mbalimbali ikiwamo sekta binafsi kuchangia mfuko huo muhimu.

Vilevile, alisema serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI pamoja na kutafuta vyanzo vya uhakika zaidi vya kutunisha mfuko huo.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kwa niaba ya serikali kuwashukuru wadau wote wa maendeleo kwa kuendelea kufanya kazi na serikali katika utekelezaji wa mikakati ya kudhibiti maambukizi mapya ya UKIMWI nchini.

"Ninawahakikishia kuwa serikali itaendelea kushirikiana nanyi katika kupambana na tatizo hili la UKIMWI," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Ajira na Wenye Ulemavu, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Ummy Nderiananga, alisema wadau wote walioshiriki katika kongamano hilo watumie ujuzi na maarifa waliyopata katika kuboresha kazi zao.

"Pia taasisi zinazojihusisha na masuala ya VVU na UKIMWI waongeze nguvu kwa kundi la wenye ulemavu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema kongamano hilo ni fursa ya kutafakari walikotoka ili waendelee kutekeleza afua za VVU na UKIMWI.

Alisema kongamano hilo linawapa fursa nzuri ya kupata takwimu zinazowasaidia kuboresha utendaji kazi ambapo ametoa mfano mwaka 2016/17 walifanya utafiti na kubaini wanaume wako nyuma katika upimaji, hivyo wanatakiwa wahamasishwe ili nao wajitokeze kwa wingi kupima.

Mwakilishi wa Mratibu Mkazi wa PEPFAR Tanzania, Dk. Hiltruda Temba, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa dhamira ya dhati ya kutokomeza VVU na UKIMWI nchini pamoja na kuendelea kutoa kipaumbele katika huduma muhimu za kinga pamoja na utekelezaji mzuri wa afua za UKIMWI.

Dk. Hiltruda pia aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa dhamira yake ya dhati ya kufikia malengo ya kuwa na asilimia 95 ya watu wanaoishi na VVU wanatambua hali zao za maambukizi, asilimia 95 ya watu wanaofahamu hali zao za maambukizi ya VVU wanapata tiba na asilimia 95 ya waliotumia dawa za ARV wamefanikiwa kupunguza kiasi cha maambukizi.

Dk. Hiltruda alisema PEPFAR na wadau wengine wa maendeleo wanaahidi kuendelea kuisaidia Serikali ya Tanzania katika kufikia malengo yake ya kimkakati kama yalivyoainishwa kwenye mkakati wa nne wa taifa wa VVU na UKIMWI.

# Wanaokula rushwa waundiwa mkakati

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuandaa sanduku la maoni na kuweka katika wizara na taasisi zote serikali ili kutoa fursa kwa wananchi na watumishi kuwabaini wala rushwa.

Vilevile, majalada 1,053 yamechunguzwa huku mengine yakiwasilishwa mahakamani kwa ajili ya kutolewa uamuzi katika kipindi cha mwaka mmoja.

Akizugumza katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa TAKUKURU wenye lengo la kutathmini utendaji kazi wao, Mchengerwa alisema juzi kuwa lengo la kuanzisha masanduku hayo ni pamoja na kutoa nafasi kwa watumishi na wananchi wanaohitaji huduma wanapoombwa rushwa, waweze kusema.

Alisema kumekuwa na tabia ya watumishi kutaka rushwa ili kuwahudumia wananchi wakati vitendo hivyo havikubaliki.

"Ninaomba suala hili likafanyiwe kazi, tunahitaji kuona jamii inapata huduma kutoka kwa watumishi bila ya bugudha yoyote," aliagiza.

Mbali na hilo, alisema serikali imetoa ajira 350 kwa TAKUKURU, hivyo wana kila sababu ya kuchapa kazi ili kuisaidia serikali kubaini wahalifu wanaopenda rushwa kazini.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna wa Polisi Salum Hamduni alisema hadi sasa taasisi hiyo imeshinda kesi za rushwa 345 na kushindwa kesi 156 huku ikiokoa Sh. bilioni 29.3.

Mbali na hilo alisema katika kipindi cha mwaka mmoja, jumla ya majalada 1,053 yamechunguzwa na kukamilika ambapo majalada 339 yaliwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kuomba kibali cha kuwafikisha mahakamani huku kesi mpya 542 zikifunguliwa katika mahakama mbalimbali kesi 541 zilitolewa uamuzi na kati ya kesi hizo Jamhuri ilishinda 345 na kushindwa kesi 156.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dua njema kwa Simba, Tembo Warriors Afrika

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Simba, wanatarajia kushuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kesho kuwakabili Red Arrows kutoka Zambia.

Mechi hiyo ni ya kwanza ya hatua ya mtoano katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, timu hizo zinatarajia kurudiana Desemba 5, mwaka huu jijini Lusaka, Zambia.

Mshindi wa jumla wa mechi hizo, atapata nafasi ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka barani Afrika.

Hata hivyo, Simba ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara watashuka uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya kuondolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tena wakiwa nyumbani baada ya kukubali kichapo cha mabao 3-1, licha ya kupata ushindi wa magoli 2-0 ilipocheza ugenini Botswana. Waswahili wanasema yaliyopita si ndwele, tugange yajayo, kwa hapa inamaana Simba inatakiwa kuachana na mawazo ya mechi hiyo iliyopita na kujipanga vyema kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo ya kwanza wakiwa hapa nyumbani.

Matokeo chanya au ushindi mnono ambao Simba wakifanikiwa kuupata kesho, utawaweka katika nafasi nzuri ya kumalizia kazi waliyoianza watakapokwenda ugenini Zambia.

Kutokana na umuhimu wa mechi hiyo na ile ya marudiano, serikali imewaomba wadau wa soka na wanamichezo nchini kuiombea Simba ushindi ili iweze kusonga mbele katika mashindano hayo kwa sababu kesho itakuwa inapeperusha bendera ya Tanzania na si ya mashabiki na wanachama wa klabu yao. Inafahamika endapo Simba atasonga mbele katika mashindano hayo, tayari itaiongezea Tanzania pointi na kujiweka kwenye nafasi ya kupata wawakilishi wanne katika michuano ya msimu ujao (timu mbili kwenye Ligi ya Mabingwa na nyingine mbili kwenye Kombe la Shirikisho).

Serikali imesisitiza mashabiki wa soka wanatakiwa kuweka pembeni itikadi zao pale wanapoona klabu ya Tanzania au timu yoyote ya taifa inapokuwa na jukumu la kupeperusha bendera ya nchi.

Tunawakumbusha wadau wa michezo, kuiombea Simba ifanye vizuri katika michuano hiyo, sio tu kutainufaisha klabu hiyo, lakini kutaendelea kulitangaza jina la Tanzania kimataifa lakini kutawasogeza pia wadhamini ambao wanahitaji kuona kiwango cha soka nchini kinapanda.

Simba itakapofanikiwa kutinga hatua ya makundi, tunaamini mawakala kutoka sehemu mbalimbali watavutika kuifuatilia timu hiyo na itakuwa ni nafasi nyingine ya wachezaji watakaofanya vyema kusajiliwa na klabu za nje kama ilivyokuwa kwa Clatous Chama na Luis Miquissone ambao wamenunuliwa na mikataba minono.

Pia huu ni wakati mwingine kwa Watanzania kuiombea dua njema Tembo Warriors (Timu ya Soka ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu), ambao leo inaanza kutupa karata yake kusaka tiketi ya kushiriki fainali za dunia.

Katika kuhakikisha Tembo Warriors inafikia malengo, na kuwa timu ya kwanza kuipeleka Tanzania kwenye fainali za dunia, Rais, Samia Suluhu Hassan, ameipatia timu hiyo Sh. milioni 150. Tembo Warriors itaanza kampeni ya michuano hiyo ya Afrika (CANAF), kwa kuvaana na Morocco, Uganda na baadaye Sierra Leone. Timu nne zitakazomaliza katika nafasi za juu zitafuzu kushiriki fainali za dunia ambazo zitafanyika mwakani nchini Uturuki. Kila la kheri Simba, Kila la kheri Tembo Warriors. Kila la kheri Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Haki ni jambo linachomstahikia mtu

Na Barnabas Maro

**HAKI** ni kitu au jambo ambalo mtu anastahiki kupata. Utendaji, ufuataji na utumiaji wa sheria na kanuni katika kutimiza jambo.

Aidha, kweli ni uhakikisho wa jambo kama lilivyo; yakini. Pia ni uimara wa hoja, bila kutetemeka; udhahiri, waziwazi, bila kusema uongo.

Ndio maana husemwa: "Kweli chungu sio uongo mtamu." Maana yake ni heri kusema ukweli mchungu kuliko uongo mtamu. Methali hii yatufunza umuhimu wa kukubali ukweli japokuwa una uchungu kuliko kushabikia uongo.

Pia huweza kutumiwa kuwanasihi watu wawe na tabia ya kusema ukweli. Watu wengine husema; "Kweli iliyo chungu si uongo ulio mtamu."

Kwa hiyo kweli ikidhihiri, uongo hujitenga. Hii ni methali inayotukumbusha ukweli wa jambo fulani utokeapo, uongo unaolihusu hautambuliwi tena au hauna nafasi tena. Huweza kutumiwa kumnasihi mtu anayejaribu kusema uongo wa waziwazi.

Wahenga walisema: "Kweli ndiyo fimbo ya kukamata." Maana yake kweli ni silaha nzuri maishani. Methali hii yatukumbusha umuhimu wa kusema ukweli hata kama kwa kufanya hivyo tutaishia kuchukiwa na wenzetu.

**Wahenga walisema: "Kweli ndiyo fimbo ya kukamata." Maana yake kweli ni silaha nzuri maishani. Methali hii yatukumbusha umuhimu wa kusema ukweli hata kama kwa kufanya hivyo tutaishia kuchukiwa na wenzetu.**

Sasa tuone zaburi inavyosema: " Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mzaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku." (Zaburi 1:1-2)

"Naye atakuwa kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; na kila alitendalo litafanikiwa." ( Zaburi 1:1-3.)

Najua kuna watakao nibeza (kitendo cha kupuuza kitu, mtu au jambo; kitendo cha kuonesha hisia ya kejeli kwa mtu; dharau; mapuuza) lakini ukweli ndo huo ila anayebisha abishe tu kwani wanadamu twatofautiana.

(Haki ni kitu au jambo ambalo mtu anastahiki kulipata. Utendaji, ufuataji na utumiaji wa sheria na kanuni katika kutimiza jambo.) Je, mwamuzi aliyechezesha mchezo wa Namungo dhidi ya Yanga kule Lindi alikuwa sahihi kuipa Yanga penalti yenye utata? Jibu ni HAPANA kwa herufi kubwa kama nilivyoandika kwani hata marejeo ya mchezo ule unathibitisha hilo!

Marudio ya mchezo kwenye luninga ya Azam yanaonyesha wazi mwamuzi wa mchezo ule hakuwa sahihi kuipa Yanga penalti ile. Kama hiyo haitoshi, hata penalti ile hakuwa makini kwani wachezaji wa pande zote mbili walikuwa katika eneo la ndani badala ya nje ya eneo hilo na kuwaacha wachezaji wawili tu - golikipa wa Namungo na mpigaji wa Yanga tu bila wachezaji wengine lakini haikuwa hivyo!

Kwa kutumia haki, Yanga haistahiki kupewa bao la kusawazisha na kuzifanya timu hizo kupata sare (suluhu) ya kufungana bao moja kwa moja.

Kweli ikidhihiri, uwongo hujitenga. Maana yake ukweli unapojulikana uongo unajitenga. Twakumbushwa kwamba ukweli wa jambo fulani utokeapo, uongo unaolihusu hautambuliwi, au hauna nafasi tena.

Sasa iweje? Bao la kusawazisha lilofungwa na Yanga lifutwe; hivyo kuwapa Namungo ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Yanga, lililofungwa kihalali.

Waamuzi wanaosababisha vurugu michezoni wasimamishwe na kurudishwa mafunzoni ili waweze kuchezesha kwa haki.

Ushindani ni tabia ya kupambana kwa maneno au vitendo bila ya kupigana.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 335 096.**

MAKALA

# KWAHERI MZEE AL NOOR KASSUM

**Patrick Rutabanzibwa***
**Mark Mwandosya****



MZEE Al Noor Kassum, maarufu "Nick" kwa marafiki zake, alifariki dunia Novemba 18 na kuzikwa Novemba 20, 2021. Pamoja na kwamba alizaliwa katika familia tajiri ya wafanyabiashara wenye asili ya Kihindi, wakati wa harakati za kutafuta Uhuru wa Tanganyika alikuwa mmoja wa watu wa karibu sana wa Mwalimu Julius Nyerere.

Baada ya uhuru aliteuliwa kuwa Waziri Mdogo wa Elimu na baada ya hapo alitumikia katika Umoja wa Mataifa kama Balozi wa UNESCO na Katibu wa Baraza la Masuala ya Kiuchumi na Kijamii (ECOSOC). Alirejea Tanzania mwaka 1970 ambapo aliteuliwa na serikali kushika nafasi ya Naibu Meneja Mkuu wa kampuni ya Williamson Diamonds, Mwadui. Baada ya hapo aliteuliwa kuwa Waziri wa Fedha na Utawala wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Jumuiya ilipovunjika mwaka 1977, Mwalimu Nyerere alimteua kuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini, nafasi ambayo aliishika kwa miaka 13 mfululizo hadi mwaka 1990 alipostaafu.

Akiwa Waziri Mdogo wa Elimu, alishughulikia uanzishwaji wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam kikiwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki. Alihusika pia na upatikanaji wa eneo la 'Observation Hill' (Mlimani) ambako kimejengwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Tulipata bahati ya kufanya kazi na Al Noor Kassum kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1980 alipokuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini. Alikuwa kiongozi mwenye upeo mkubwa: Mchapakazi; mfuatiliaji sana wa utekelezaji wa kazi; mtu aliyependa kuwahamasisha watendaji kuiga mwenendo wake badala ya kuwashurutisha; mwenye kipaji cha kujenga ushirikiano wa karibu kati ya wote aliowaongoza; na aliyesikiliza na kuthamini ushauri wa wataalamu bila kujali umri wao wala vyeo vyao.

Aliheshimu sana sheria na taratibu zote husika katika utekelezaji wa majukumu yake. Uzalendo wake haukuwa wa kujinadi. Ulijidhihirisha katika vitendo, siyo maneno.

Kwa lengo la kukabiliana na changamoto za sekta ya nishati zilizojitokeza duniani kote mwishoni mwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980, alijenga hoja serikalini ya kuanzisha idara maalumu ya kushughulikia na kuratibu masuala yote ya nishati. Yeye binafsi alihusika katika kujenga timu ya kufanikisha lengo hilo.

Alimtafuta mhadhiri mmoja kijana wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye alikuwa anafundisha na kufanya utafiti juu ya masuala ya nishati, akamchukua kuwa mshauri wake, na baadaye akapendekeza Rais Julius Kambarage Nyerere amteue kuwa kamishna wa masuala ya Petroli kwa mujibu wa sheria. Hivyo ndivyo Prof. Mark Mwandosya alivyoteuliwa kuwa Kamishna wa kwanza wa Nishati na Petroli na Mkuu wa Idara ya Nishati.

Vilevile, alimwazima kijana mwingine kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na kumfanya msaidizi wake katika kufuatilia miradi ya mafuta na gesi, na baada ya kumpa uzoefu katika ufuatiliaji na uratibu akamhamishia katika Idara ya Nishati. Ndivyo Patrick Rutabanzibwa alivyokuja kuwa msaidizi mmojawapo wa Mark Mwandosya mwaka 1985 na kuteuliwa katika nafasi yake ya Kamishna wa Nishati na Petroli baada ya Mark Mwandosya kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini mwaka 1990.

Juhudi za Waziri Kassum za kuijenga na kuiwezesha Idara ya Nishati kupata rasilimali watu hazikuishia hapo. Alielekeza vijana wengine wahandisi wa Idara ya Maji wenye uwezo mkubwa, Bashir Mrindoko, Estomih Sawe na Shaban Mgana, wahamishiwe kwenye idara ya Nishati.

Aidha, alimvuta kijana mwingine, Theodore Kapiga, mchumi, kutoka Mamlaka ya Bonde la Mto Rufiji (RUBADA) kujiunga na Idara, pamoja na mhandisi, Vincent Gondwe (sasa marehemu) ambaye kabla ya kuanzishwa kwa Idara ya Nishati alikuwa akishughulikia masuala ya nishati akiwa katika Idara ya Sera na Mipango ya Wizara.

Baada ya kuanzishwa ikiwa na watendaji hao wachache, idara ya Nishati iliendelea kukua na kuongeza uwezo wake wa kusimamia utekelezaji wa sera, mikakati na mipango ya uendelezaji wa sekta ya nishati. Prosper Victus, Lutengano Mwakahesya, Ngosi Mwihava, Theophillo Bwakea na Charles Omujuni ni baadhi tu ya watendaji walioajiriwa idara ilipokuwa changa kabisa na baadaye wakahamishiwa na kutoa mchango mkubwa katika taasisi zingine za serikali zilizo ndani na nje ya sekta ya nishati.

Waziri Kassum alijenga uhusiano mzuri wa kikazi na mawaziri wenzake pamoja na Makatibu Wakuu wake Frederick Lwegarulila (marehemu); Harith Bakari Mwapachu (marehemu); Athumani Janguo; Fulgence Kazaura (marehemu) na Paul Mkanga.

Uhusiano huo uliwezesha uamuzi juu ya masuala mbalimbali ya wizara yake kufikiwa na kutekelezwa kwa ufanisi. Pia alitumia uzoefu wake katika mahusiano ya kimataifa kuwashawishi washirika wa maendeleo kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya nishati na kugharimia wataalamu washauri kutoka nje ya nchi ambao waliletwa katika Wizara na mashirika yake kuwasaidia watendaji kushughulikia masuala ya uendelezaji wa umeme, mafuta na gesi, na nishati jadidifu.

Baadhi ya wataalamu hao – kwa mfano Roger Nellist kutoka Uingereza (aliyeletwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola), Sigurd Heiberg na Farouk Al Kasim kutoka Norway (walitoka Statoil na Norwegian Petroleum Directorate), Dr. Kokitil Narayanan kutoka India (Oil & Natural Gas Commission) na Paul Precht kutoka Canada (Canadian International Development Agency) – waliendelea kujihusisha na juhudi mbalimbali za kuendeleza rasilimali watu katika Idara ya Nishati, TPDC na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa miaka mingi baada ya kurejea katika nchi zao.

Idara ya Nishati ilijenga utamaduni ambao uliipa sifa ya kuwa moja ya idara za serikali zilizokuwa na watendaji wachapakazi, wawazi na weledi. Mwaka 2004, wakati mrithi wa Waziri Kassum, Jakaya Kikwete, alipokabidhi ofisi ya Waziri wa Maji, Nishati na Madini kwa mrithi wake, Jackson Makwetta (marehemu), alimtahadharisha kwamba idara hiyo ina watendaji wabishi sana lakini wako makini, na ole wake apuuze ushauri wao.

Kwa kiasi kikubwa tahadhari hiyo ilitokana na uongozi bora wa Waziri Kassum, ambaye aliwaandaa na kuwaendeleza kiutendaji maofisa wengi wa Idara waliopata fursa ya kufanya kazi naye.

Hivyo basi, si jambo la kushangaza kwamba Waziri Kassum alichangia maendeleo ya sekta za maji, nishati na madini kwa kiwango tunachokishuhudia hadi leo na kuacha urithi wa kudumu.

Yafuatayo ni baadhi tu ya mambo muhimu aliyoyafanya wakati alipokuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

• Alipitisha Bungeni Sheria ya Madini (1979) na ya Petroli (1980) ambazo ziliweka mazingira ya sekta binafsi kushiriki zaidi katika utafutaji na uzalishaji wa madini, mafuta na gesi wakati nchi yetu ilipokuwa inaendeshwa kwa sera za ujamaa. Alionekana kuishi kabla ya wakati wake. Andrew Chenge, wakati huo akiwa ofisa mwandamizi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, alitoa mchango mkubwa katika maandalizi ya sheria hizo.



Marehemu Mzee Al Noor Kassum (katikati) enzi za uhai wake, akiwa na Prof, Mwandosya (kushoto) na Patrick Rutabanzibwa (kulia)

INAENDELEA UK. 15

# Waziri ataka kasi makusanyo kodi ya pango

**Na Munir Shemweta, WANMM KAHAMA**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameitaka Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga kuongeza kasi ya ukusanyaji kodi ya pango la ardhi.

Hatua hiyo inatokana na Dk. Mabula kutoridhishwa na kasi ya ukusanyaji mapato yatokanayo na kodi ya ardhi. Manispaa hiyo hadi Novemba, mwaka huu, imekusanya Sh. 460,328,934 kati ya Sh. bilioni 3.5 ilizopangiwa kukusanya katika mwaka wa fedha 2021/22.

Kwa mujibu wa Ofisa Ardhi Mteuli Manispaa ya Kahama, Yusufu Luhumba., katika kipindi cha mwaka wa 2020/21 Halmashauri ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 2.5 lakini ilikusanya Sh. bilioni 1.330 sawa na asilimia 53.25.

Aidha, Manispaa hiyo inawadai wamiliki wa ardhi Sh. bilioni 1.6, hivyo Naibu Waziri akaelekeza manispaa hiyo kuhakikisha inawachukulia hatua wote walioshindwa kulipa madeni ya kodi ya pango kwa wakati kwa kuwa wamevunja masharti ya umiliki.

Hata hivyo, Dk. Mabula aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi kabla ya kuwafikisha wadaiwa katika mabaraza ya ardhi, kuzungumza nao ili kuangalia namna bora ya kulipa madeni hayo na kuongeza kuwa iwapo wako wadaiwa wanaoweza kulipa kwa awamu, mazungumzo yafanyike lakini kwa kuzingatia fedha kulipwa kipindi cha mwaka wa fedha husika.

Akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi katika Manispaa ya Kahama akiwa katika ziara yake ya siku mbili katika Mkoa wa Shinyanga juzi, Dk. Mabula alisema wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi walioshindwa kulipa madeni yao, wanatakiwa kufikishwa katika mabaraza ya ardhi ili washtakiwe kwa kushindwa kulipa. "Maelekezo yangu wale wote walioshindwa kulipa madeni yao, sheria ichukue mkondo wake ikiwemo kuwafikisha katika mabaraza ya ardhi ambako huko uamuzi ni kulipa au mali za wahusika kupigwa mnada kufidia deni," alisema Dk. Mabula.

Aidha, Dk. Mabula aliitaka Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kuhakikisha inatumia vyombo vya habari na ujumbe wa simu kuwakumbusha wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya pango kwa wakati na kuiwezesha serikali kupata mapato. Awali, Ofisa Ardhi Mteule, Yusufu Luhumba, alisema Halmashauri ya Manispaa ya Kahama imeendelea na utaratibu wa kuwafuatilia wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi na thamini 37 za wadaiwa kati ya 103 zimekwishakabidhiwa kwa dalali wa mahakama kwa utekelezaji.

"Wakati thamini 54 zimekwisha andaliwa na kukamilika, kwa sasa zinasubiri kusainiwa na mthamini Mkuu wa serikali kisha kupelekwa kwa dalali wa mahakama kwa utekelezaji wa uuzaji," alisema Luhumba.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (katikati), akiteta jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Coca-Cola Kwanza Tanzania, Unguu Sulay (kushoto), wakati wa kilele cha tamasha la 'Biriani Festival na Coca-Cola', katika viwanja vya Posta, Kijitonyama mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii, ambalo ni sehemu ya shamrashamra za kampeni mpya ya 'Maajabu Halisi.' Kulia ni Mkurugenzi wa Masuala ya Umma na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Salum Nassor. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yatoa mikopo bil. 70/- kwa wachimbaji

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

BENKI ya NMB imetoa zaidi ya Sh. bilioni 70 ndani ya mwaka mmoja kwa ajili ya mikopo nafuu ya kusaidia wachimbaji wadogo na wakubwa na imekuwa chachu ya ukuaji wa hatua kubwa katika sekta ya madini nchini.

Mkuu wa Idara ya Biashara wa NMB, NMB, Alex Mgeni, alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa klabu ya wachimba madini mkoani Morogoro ambapo NMB imekuwa benki ya karibu zaidi kwa sekta ya madini na ndiyo iliyofikia wadau wengi zaidi wa sekta ya hiyo. Hatua hiyo imewezesha benki hiyo kutoa mikopo ya zaidi ya Sh. bilioni 70 ndani ya mwaka mmoja.

Mgeni alisema benki hiyo inatambua changamoto kubwa ya mitaji na gharama kubwa za mitambo ya kuendeshea shuguli za madini na imeweka mikopo ambayo ni rafiki kwa wateja ili wasikwame katika shuguli zao.

"Katika kipindi cha mwaka mmoja tu, tayari watu katika sekta ya madini wamenufaika na mikopo yetu. Zaidi ya Sh. bilioni 30 zimeelekezwa kwa wachimbaji wadogo na zaidi ya Sh. bilioni 40 kwa wachimbaji wakubwa," alisema.

"Tumezunguka sehemu mbalimbali ambako shuguli za madini zinafanyika na kiukweli tumeshuhudia namna ambavyo mikopo hii imekuwa chachu ya kukua kwa sekta hii ya madini," aliongeza.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, aliipongeza benki hiyo kwa hatua kubwa ya kuja na Klabu ya Madini ya NMB na kuwajali wadau wa sekta ya madini kwa kuwa wamekuwa wakisahaulika na taasisi zingine za fedha na kuwaweka katika kundi la watu wasiokopesheka.

"Niwapongeze sana NMB kwa kuwajali watu wa madini kwani mara nyingi wamekuwa kundi gumu sana kukopesheka. Nyie mmechagua kufanya kazi na kundi hili ambalo ni la muhimu kwa uchumi wa taifa letu," alisema Msando.

Msando ambaye alimwakilisha mkuu wa mkoa huo, alisema wadau wa sekta ya madini wawe na mifumo rasmi ya utunzaji wa fedha zao na kumbukumbu za biashara zao ili iwe rahisi kwao na kwa benki kufanikisha mikopo yao ndani ya muda mfupi.

Akizungumza kwa niaba ya wachimbaji, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wachimbaji Mkoa wa Morogoro, Dk. Nivuka Mzeru, alipongeza uundaji wa 'NMB minning Club' kwa kuwa itaenda kutatua changamoto kubwa ya wachimbaji wengi ya mitaji na vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi.

NMB Minning Club imezinduliwa rasmi mkoani Morogoro na kuungana na mikoa mingine kama Dodoma, Mwanza, Shinyanga na Arusha ambako tayari klabu hizi zimeshazinduliwa na kuwaweka wadau wa sekta ya madini pamoja na benki ya NMB karibu.

## Mafunzo yatolewa kudhibiti sumukuvu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imeanza kutoa mafunzo kupitia Mradi wa Kitaifa wa Kudhibiti Sumukuvu "Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination (TANPACK)" yatakayotolewa katika wilaya 18 na mikoa 10 nchini.

Mafunzo ya mradi huo yalizinduliwa rasmi juzi Kiteto mkoani Manyara na kuhudhuriwa na washiriki 120. Mradi huo uko chini ya Wizara ya Kilimo na TBS imekabidhiwa jukumu la kutoa mafunzo hayo.

Akizungumzia na waandishi wa habari wilayani humo kuhusu wilaya na mikoa itakayonufaika na mafuzo hayo, Jabir Abdi wa TBS alitaja wilaya hizo kuwa ni za Kondoa, Chemba, Bahi, Kongwa, Babati, na Kiteto.

Wilaya zingine ni Namtumbo, Newala, Nanyumbu, Nzega, Urambo, Kibondo, Kasulu, Buchosa, Bukombe, Itilima, Kilosa na Gairo. Kuhusu mikoa ziliko wilaya hizo, Abdi alisema ni Dodoma, Manyara Ruvuma, Mtwara, Tabora, Kigoma, Mwanza, Geita,Simiyu na Morogoro.

Aliwataja walengwa wa mafunzo hayo kuwa ni wafanyabiashara, wasafirishaji na wasindikaji wa mahindi na karanga pamoja na bidhaa zake.

Abdi alitaja faida za mafunzo kuwa yanalenga kulinda afya za binadamu, kuwezesha biashara ya mazao ya mahindi na karanga, kulinda afya za mifugo na kuwezesha utoshelevu wa chakula salama.

Faida nyingine, alitaja kuwa ni kuhimili ushindani katika masoko ya ndani, kikanda na nje ya nchi.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Mbaraka Alhaji Batenga, alipongeza uamuzi wa serikali kuanzisha mafunzo hayo kwa sababu chakula ni hitaji muhimu kwa binadamu na ustawi wa maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Hata hivyo, alisema usalama wa chakula unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa sumukuvu ambao husababisha madhara ya kiafya na hata kiuchumi.





## Serikali kushirikiana kamati ya maridhiano

**Na Peter Mkwavila,** MPWAPWA

SERIKALI imesema itaendelea kufanya kazi kwa pamoja na Jumuiya ya Maridhiano katika shughuli zake za kimaendeleo ikiwa ni pamoja na kutatua migogoro inayojitokeza kwenye jamii na taasisi mbalimbali za kidini.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mpwapwa, Sarah Komba, alisema hayo alipokuwa akizungumza na viongozi wa Jumuiya ya Maridhiano wa mkoa na wilaya ofisini kwa mkuu wa wilaya ya Mpwapwa.

Alisema serikali ina kila sababu kufanya kazi kwa pamoja kutokana na mchango mkubwa unaotolewa na kuonyeshwa na jumuiya hiyo ya maridhiano ikiwamo katika kuisaidia serikali kutatua migogoro inayoibuka.

Pia alisema kuna migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza kwenye taasisi za kidini na kijamii na hata kuhatarisha amani.

"Lakini tumeshuhudia jumuiya hiyo ikiimaliza kwa kupatanisha kwa amani kupitia vikao vyake vya maaridhiano.

"Mimi mwenyewe hapa Mpwapwa nimeshuhudia moja ya taasisi za kidini waumini wake walifikia sehemu hata ya kuhatarisha amani, lakini kwa juhudi za serikali na vioongozi wa dini walitatua na hali ikawa ya utulivu, amani, upendo na mshikamano"alisema

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo ya maridhiano Mkoa wa Dodoma, Dk. Evance Chande, alisema moja ya majukumu yake ni kuhakikisha amani inatawala.

Hata hivyo, aliihakikishia serikali kuwa jumuiya hiyo ya maridhiano itaendelea kufanya kazi kwa pamoja bila kujali itikadi yoyote ikiwamo ya kidini, kabila siasa na rangi.

Awali akizungumza na viongozi wa wilaya hiyo ya Mpwapwa aliwataka kutofanya kazi zao kwa mazoea badala yake wafuate utaratibu kwa mujibu wa katiba.

Naye Mwenyekiti wa jumuiya ya maridhiano Wilaya ya Mpwapwa, Shekhe Hassani Chilogasa, aliomba elimu zaidi ipelekwe vijijini ili wananchi waweze kuishi kwa amani na ushirikiano.

# Maaskofu Pentekoste waibua tena tozo za miamala ya simu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI Tendaji ya Halmashauri Kuu ya Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), imeiomba serikali kuwapunguzia wananchi gharama za tozo ya miamala ya simu wakati huu ambapo kuna tishio la njaa.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Askofu Peter Konki, alitoa ombi hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya kamati hiyo.

"Tumekuwa hapa na kikao cha Kamati Tendaji ya Halmashauri Kuu ya CPCT. Wajumbe wengine wameshaondoka lakini sisi baadhi tumebaki ili kuzungumza nanyi kuhusu jambo hili," alisema.

Konki alisema hivi sasa kumekuwapo na ukame wa muda mrefu katika maeneo mengi ya nchi hali ambayo inatishia uwapo wa baa la njaa.

Alisema kutokana na hali hiyo, wanaiomba serikali kuangalia namna ya kuwapunguzia wananchi gharama za tozo za miamala ya simu ili kumudu gharama za maisha wakati huu wa ukame.

"Katika maeneo mengi nchini hivi sasa hakuna mvua kabisa hali inayotishia kuwapo na ukame utakaosababisha njaa kutokana na uhaba wa mvua katika msimu huu wa kilimo.

"Wakati kama huu katika maeneo yote nchini ndiyo wananchi huwa wameanza kupanda lakini pia hata majani huwa yameanza kuota lakini mpaka sasa hakuna hata mboga za majani katika maeneo mengi," alisema.

Pia aliishauri serikali kuhamasisha wananchi kuhifadhi chakula walicho nacho majumbani badala ya kukitumia ovyo.

"Hatuwezi kujua hali hii itakuwaje na itakuwa hivi hadi lini, hivyo tunapenda kuishirikisha serikali kutoa elimu kwa wananchi wake kuhifadhi chakula walichonacho majumbani,' alisema.

Kadhalika, aliisihi serikali kutunza chakula ambacho kipo katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa ajili ya tahadhari ya ukame unaoendelea sasa nchini.

"Hatuwezi kutegemea kulisha watu wetu kwa chakula cha msaada kwani hatufahamu baa la njaa litakuwa na ukubwa wa kiasi gani na huu ukame utadumu hadi lini," alisisitiza Askofu Konki

Vilevile, alisema kutokana na hali hiyo CPCT imeandaa maombi maalumu ya kufunga na kuomba kwa muda wa siku 14, kuombea hali hiyo.

"Nitumie fursa hii kuwaalika wanachama wa CPCT na Watanzania kwa ujumla kuungana nasi kushiriki maombi haya yatakayoanza Desemba Mosi hadi 14 mwaka huu ili kumwomba Mungu atuepushie na hali hii," alisema Askofu Konki




Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, wakati akiwasilisha taarifa ya mafanikio na mwelekeo wa wizara hiyo, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# MAT yatoa mwongozo malalamiko kwa madaktari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Madaktari Tanganyika (MAT) limetoa ufafanuzi kwa jamii kuhusu utaratibu wa kuwasilisha malalamiko ya ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma kwa kada hiyo.

Ufafanuzi huo ulitolewa jana jijini hapa na Msajili wa Baraza hilo, David Mnzava, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzingatiaji wa maadili ya kiutumishi kwa madaktari, madaktari wa meno na wataalamu wa afya shirikishi.

Mzava alisema mlalamikaji anaelekezwa kuwasilisha shauri lake kwenye ofisi ya msajili wa baraza au kupitia mamlaka za usimamizi za wilaya na mikoa.

"Mamlaka hizi kwa kupitia kamati zake zina wajibu wa kufanya uchunguzi wa awali na kuwasailisha kwa msajili taarifa ya mashauri waliyoyachunguza na uamuzi wa kamati ikiwa ni shauri dogo na ikiwa ni shauri kubwa kuwasilisha mapendekezo yao kwa baraza," alisema Mzava.

Pia alisema uamuzi wa mamlaka hizo unatakiwa uwasilishwe kwa maandishi kwa mlalamikaji ukiambatana na maelekezo ya ukataji wa rufani kwenye ofisi ya msajili kwa ambaye hajaridhika na uamuzi huo.

"Kwa makosa makubwa, wataalamu waliohusika watapatiwa notisi ya uchunguzi wa awali ambayo wataijibu ndani ya siku 14," alifafanua Mnzava

Kadhalika alisema baada ya taarifa ya uchunguzi wa awali kutoka taratibu zinazofuata za uchunguzi zitaendelea kwa mujibu wa sheria.

Alisema baraza linatoa wito kwa wasimamizi wa mikoa na wilaya kuweka mipango thabiti ya kusimamia utendaji wa wanataaluma katika maeneo yao.

Vilevile, kuweka utaratibu mzuri wa kutoa mrejesho kwa walalamikaji na kuwaeleza haki yao ya kukata rufaa kwa baraza pale ambapo hawajaridhika na uamuzi wa kamati za vituo vya wilaya na mikoa.

"Misingi ya taaluma ya udaktari, udakatari wa meno na utaalamu wa afya shirikishi inajengwa na kanuni za maadili za wanataaluma zilizoainishwa katika kanuni za maadili na utendaji wa kitaaluma kwa madakatari za mwaka 2005," alisema.

Msajili alisema kanuni hizo zimeanishwa katika mchanganuo wa kanuni kuu tano ikiwamo ya wanataaluma kutenda wema kufanya ubinadamu.

"Mwanataaluma ana wajibu wa kutoa huduma ya dharura na kutoa huduma inayoendana na ushahidi wa kisanyansi mfano matumizi ya miongozo ya kutolea huduma na kutumia majibu ya vipimo kwa usahihi na kwa wakati kujua na kuamua yanayofaa kwa wagonjwa," alisema.





# Rais Mwinyi ataka ufumbuzi kero ya maji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameiagiza Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kulipatia ufumbuzi tatizo la maji kwa baadhi ya maeneo ya mji wa Zanzibar ili wananchi waendelee kupata huduma hiyo ipasavyo.

Dk. Mwinyi alitoa agizo hilo jana alipotembelea na kukagua vyanzo vya mradi wa maji unaopeleka huduma hiyo mjini Zanzibar ambao miundombinu yake imeharibika. Hatua hiyo imesababisha kukosekana kwa huduma hiyo katika maeneo mbalimbali ya mji wa Zanzibar.

Rais Mwinyi aliwataka watendaji wa ZAWA kuongeza kasi katika utatuzi wa kero ya maji inayoukabili mji, akibainisha matumaini yake baada ya baadhi ya vifaa, yakiwamo mabomba kuwasili.

Pia ZAWA kutengeneza mfumo utakaowawezesha wananchi wa maeneo ya Miwani, Kizimbani na Bumbwisudi kupata huduma za maji kupitia mradi wa maji safi na salama unaopeleka huduma hiyo mjini Zanzibar.

Alisema kuna umuhimu wa ZAWA kuandaa mfumo maalum kutoka kisima kimoja miongoni mwa visima saba vilivyopo, ili wananchi wa maeneo hayo kupata huduma hiyo ya maji.

Mradi huo, alisema wakati unaanzishwa haukuzingatia mahitaji ya wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka vyanzo hivyo, na hivyo kuwafanya kukosa kabisa huduma hiyo.

Pia alisema serikali hivi sasa ina mpango wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya barabara na umeme, hivyo akawahakikishia wananchi wa maeneo hayo kuwa Serikali itashughulikia changamoto zinazowakabili.

Dk. Mwinyi aliwataka wananchi hao kuwa wastahamilivu katika kipindi hiki cha kiangazi, sambamba na kuwataka kumwomba Mungu ili awaletee neema ya mvua na kuendeleza kilimo mashambani.

Pia aliwashukuru mafundi wa ZAWA kwa kufanikiwa kurejesha mfumo uliosababisha kuanguka kwa mabomba na kusababisha ukosefu huo wa maji.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA, Dk. Salha Mohamed Kassim, alisema kazi kubwa zinazofanywa na mamlaka hiyo zinahitaji gharama kubwa na kubainisha mpango maalum ulioandaliwa wa kulipa madeni, yakiwamo ya walinzi wa kiraia kwenye visima vya maji. Aliwahakikishia wananchi hao kuwa wale wote wanaoidai mamlaka hiyo watapatiwa haki zao hivi karibuni.

Baadhi ya wananchi wanaoishi karibu na vyanzo hivyo, walionyesha masikitiko yao kwa kukosa huduma za maji safi na salama kwa kipindi chote tangu mradi huo unaopeleka maji Mjini kuanzishwa, ingawa vyanzo vya huduma hiyo inapatikana katika maeneo yao.

Pia walilalamika kuwapo kwa barabara mbovu kuelekea katika shehiya zao pamoja na ukosefu wa huduma za umeme, kero ambazo Rais Dk. Mwinyi aliwahakikishia zitapatiwa ufumbuzi.



Mwanaharakati wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ali Makame Issa, akizungumza na waandishi wa habari jijini Zanzibar jana, kuhusu bodi ya udhibiti wa vileo Zanzibar kufanya kazi bila ya kuzingatia uwazi hasa katika utoaji wa zabuni za uingizaji wa vileo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bodi vileo yatakiwa uwazi utendaji kazi

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar, (ZLB) imetakiwa kufanya shughuli zake kwa uwazi ikiwamo kuweka wazi kampuni zilizojitokeza kuomba kibali cha uingizaji wa Pombe Visiwani Zanzibar.

Wito huo ulitolewa jana na mwanaharakati wa haki za binadamu za utawala bora, Ali Makame Issa, wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar kuhusu bodi mpya iliyoteuliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

"Tunaomba bodi ya vileo ifanye shughuli zake kwa uwazi. Tumeshughudia bodi imeundwa kimyakimya baada ya kuteuliwa Mwenyekiti na mchakato wa utoaji wa zabuni kwa kampuni zinazotakiwa kuingizwa vileo mwaka wa fedha 2021/22 mpaka sasa haujatangazwa kinyume cha sheria," alisema.

Alisema mwaka wa fedha wa 2020/21 zabuni ilitangazwa Oktoba na kampuni zikajitokeza baada ya matangazo kupitia vyombo vya habari lakini sasa mwaka unamalizika zabuni haijatangazwa.

"Wananchi wanapaswa kufahamu viongozi wa bodi ya udhibiti wa vileo Zanzibar na kampuni zilizojitokeza kuomba uingizaji wa vileo Zanzibar ili Wananchi wapate kufahamu badala ya mchakato kufanyika kimyakimya.

Makame alimpongeza Rais Mwinyi kwa kuivunja bodi ya zamani ya vileo baada ya kuvunja sheria namba 9 ya mwaka 2020 kuhusu zaidi ya kampuni tatu kwa kutoa vibali vya kuingiza vileo Zanzibar kinyume cha Sheria ya Vileo namba 33(1) ya sheria hiyo.

"Tunazo taarifa kuna hadi wawekezaji wa kizungu wameanza kuingiza vileo Zanzibar kinyume na masharti ya sheria kama inavyoelezwa katika kifungu cha 33(1) mmiliki wa kampuni ya uingizaji vileo lazima awe Mzanzibari, awe mlipakodi, awe na ghala la kuhifadhia na magari ya kusambaza vileo," alisema mwanaharakati huyo.

Alisema wakati umefika wa mamlaka za kupambana na rushwa na uhujumu wa uchi kuchunguza kwa karibu kampuni zinazopewa uingizaji wa vileo Zanzibar kutokana na sheria kuendelea kuvunjwa.

Hivi karibuni, Katibu wa Bodi, Zainab Makame Sururu, alithibitisha kuundwa kwa bodi mpya lakini hakuwa tayari kuzungumza kwa madai ya kwamba msemaji ni mwenyekiti wa bodi hiyo.

# Rais asema kushamiri vitendo udhalilishaji ni aibu kwa nchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema pamoja na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa bado vitendo vya udhalilishaji vinaendelea kuwa jambo la aibu Zanzibar.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema hayo juzi kupitia hotuba aliyosoma kwa niaba ya Rais Dk. Mwinyi katika ufunguzi wa kongamano la maadhimisho ya siku 16 za kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto lililofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar.

Alisema vitendo hivyo vimekuwa vikiendelea kutokea kupitia sura tofauti ikiwamo kupigwa kwa wanawake, kutelekezwa kwa watoto, talaka zisizofuata utaratibu, ndoa za umri mdogo, sambamba na ushirikishwaji wa watoto wenye umri mdogo katika biashara zisizokuwa rasmi.

Hemed alisema ni jambo la kushangaza katika jamii ya leo kwa baadhi ya wazazi kuacha majukumu yao ya msingi ya malezi na ulinzi wa familia badala yake kujiingiza katika vitendo vya udhalilishaji jambo ambalo linaashiria ukatili uliokithiri kwa wazazi wenye mila na desturi za kistarabu kuwafanyia watoto.

Alisema kuna kila sababu kwa wazazi wenye tabia hizo kuacha mara moja ili watoto waondokane na kadhia hiyo inayowakumba siku hadi siku na kuwanyima furaha na amani katika maisha yao yote.

Pia aliwataka wazazi na walezi kubadilika kulingana na wakati katika kuangalia kwa kina malezi ya watoto kwa lengo la kuwawezesha watoto kupambanua mambo yanayofaa na yasiofaa huku akitolea mfano kitendo cha wazazi kuwaacha watoto nyumbani pekee yao na wao kujikita katika shughuli nyingine na kuacha jukumu lao la malezi.

" Ndugu wazazi na walezi ulezi wa namna hii umeshapitwa na wakati , ulezi kama huu unatoa fursa kwa wahalifu kufanya vitendo vya udhalilishaji kwa watoto wetu," alisema Hemed

Alibainisha kwamba kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, vitendo vya udhalilishaji vimekuwa vikiripotiwa katika wilaya zote za Zanzibar na Wilaya za Mkoa wa Mjini Magharibi zinaongoza kuwa na idadi kubwa ya vitendo hivyo.

Alisema kwa kipindi Januari hadi Septemba, mwaka huu, matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia 928 yameripotiwa, wanawake 126 na watoto 802 na Wilaya ya Magharibi "A" ina idadi kubwa ya matukio ukilinganisha na wilaya zingine.

Hemed alisema matukio hayo yanajumuisha kubakwa 468, kulawitiwa 140, kuingiliwa kinyume cha maumbile 52, kutorosha 79, shambulio la aibu 88 na shabulio 106.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuchukua jitihada mbalimbali kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji ikiwamo kuimarisha mifumo ya kisheria kwa kuweka mahakama maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji na kuongeza mahakimu ili kupunguza mlundikano wa kesi ambao ulikuwa kilio kikubwa kwa wananchi.

Alisema tangu kuanzishwa kwa mahakama hiyo jumla ya kesi 345 zimeripotiwa kuanzia Febuari 2021 hadi Oktoba, mwaka huu 2021 na kesi 78 zimepatiwa uamuzi na kueleza kuwa kupitia mahakama hiyo kesi zimekuwa zikichukua muda mfupi kupatiwa hukumu na bado serikali inaendelea na msimamo wake wa kuhakikisha kesi hizo hazina dhamana hali ambayo inawajengea hofu wahalifu wa vitendo hivo.

Naye Waziri wa Afya Ustawi wa Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema lengo la kuwapo kwa maadhimisho ya hayo ni kufanya tathmini na kujadili juhudi za wadau mbali mbali juu ya masuala ya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia pamoja na kupanga mikakati thabiti itakayoweza kutoa mwongozo juu ya kupunguza matendo hayo.



**PRIYANKA HIVI JONAS KAKUTALIKI?** Ukurasa.14

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI NOVEMBA 27, 2021



## 'UKINIZINGUA TUTAZINGUANA'

# Wolper atoa mkwara mzito

MSANII mkongwe wa filamu nchini, Jackline Wolper, ameweka wazi kwamba siku atakapotambua baba mtoto wake Rich Mitindo amemuumiza, dunia yote itatambua kwani hana tabia ya kuweka siri kwa jambo hilo.

Akizungumza na EATV, Wolper amesema moyo wake hauna uvumilivu pale anapoumizwa na endapo itatokea hali hiyo hatamuacha mzazi mwenzake salama.

Amesema yeye na Rich wamekutana kila mtu akiwa na kazi yake ya mitindo, hivyo anatarajia wataendelea kuishi kwa kupendana, kuaminiana na kusaidiana kutokana na kumfanyia makubwa katika maisha yake.

Wolper ameeleza kwamba hata alipojifungua mtoto wake, aliamua kutumia njia ya kawaida ili kupata uchungu wa mwanamke na hilo ni jambo pekee linalotakiwa kuheshimiwa.

"Nilipojifungua P niliingia leba kwa uchungu, sikutaka kufanyiwa upasuaji ili nipate uchungu wa mwanamke, hivyo ni lazima aniheshimu na kama ikitokea ameniumiza nakwambia hatatoka salama lazima kila mtu atajua," amesema.

Hata hivyo, amesema katika maisha yao wanaepuka kupokea maneno ya pembeni ili kuepuka umbea ambao unaweza kuwatenganisha.

"Mimi nina baba wa mtoto wangu unaponiletea maneno unataka nizae na mwanamume gani mwingine, sitaki kuwa na watoto wenye baba tofauti na ndio maana tunaepuka maneno ya nje," ameongeza.

Amewataka wanawake kuacha tabia ya kuvumilia mateso kwa sababu tu, mwanamume ana pesa nyingi kwani jambo hilo linawadhalilisha na kuwaondoa utu.

BASI SAWA

## Mos P aitakia 'Nchi Yetu'mshikamano

MWANAMUZIKI chipukizi, Amos Ntenga maarufu kama Mos P, ametambulisha wimbo wake mpya 'Nchi Yetu' ambao ni maalum katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru.

Akizungumza na BT, Mos P amesema kibao hicho kimerekodiwa katika studio ya New Sound ya jijini Dar es Salaam na tayari kimeanza kuchezwa katika vituo mbalimbali vya redio.

"Huu ni wimbo wangu wa kwanza kuutambulisha ni maalumu kwa ajili ya kuwaenzi viongozi wetu ambao wamefanya kazi kubwa kupigania taifa letu na kuleta maendeleo," amesema




## Pacha' wa Billnas kweli kiboko



MSANII wa Bongo Fleva aliyejizolea umaarufu kwa kufanana na Billnas, Carly Npagafinyu, ameendelea kupenya kwenye masikio ya mashabiki kupitia ngoma yake, 'Shuka' aliyomshirikisha M.M.S.

Msanii huyo anayefahamika kama Carly Boy, amesema kamwe hawezi kutembelea nyota ya staa huyo, badala yake kazi anazozifanya ndizo zitamtambulisha kwa mashabiki.

Aidha ameeleza kuwa anashukuru kuona ngoma yake inafanya vizuri na kupata maoni mengi ya kumpa moyo kutoka kwa wapenzi wa muziki.



## Mobeto tuambie kama Ross ni shemeji?

TANGU juzi kuna picha zinasambaa kutoka Dubai, Falme za Kiarabu, juu ya mwanamitindo maarufu Hamisa Mobetto akiwa kwenye bonge moja la klabu akicheza muziki na rapa maarufu nchini Marekani, Rick Ross.

Mitandao mbalimbali ya kijamii imekuwa ikisambaza picha hizo, ambapo wengi wanahisi kuwa si bure huenda kuna jambo.

Hivi karibuni, Mwijaku alisema kuwa Hamisa amepata mchumba na anatarajia kuolewa, lakini mchumba mwenyewe si Mtanzania na wala hatoki nchi yoyote barani Afrika.

Inadaiwa kuwa Rick yupo nchini humo kwa ajili ya ziara ya muziki, huku Mobetto akiwa kwenye shughuli zake za kibiashara.

Mwenyewe Mobetto ameweka video hiyo na kuandika kwenye mtandao wake 'dad is here'.



## Dimpoz akoleza joto

MASHABIKI wa muziki wamezidi kupata joto, baada ya mwanamuziki wa Bongofleva, Ommy Dimpoz na mkali wa bolingo, Fally Ipupa, kutangaza ujio wa ngoma yao mpya.

Tangu Dimpoz aweke kwenye ukurasa wake wa Instagram, kuwa watu wategemee kazi yake mpya akishirikiana na fundi huyo wa muziki Afrika, mjadala unazidi kupamba moto kutaka kuona kama ngoma hiyo itakuwa kali zaidi ya aliyofanya Diamond na mwanamuziki huyo.

Diamond na Fally Ipupa, walifanya kazi ya pamoja mwaka mwaka 2019 na kufanikiwa kuwapagawisha mashabiki wao.

## Ya Gigy yaache yapite

**Na Adam Fungamwango**

MAISHA ni maisha tu, awe ni mtu wa kawaida au maarufu, wote wako kwenye dunia hii hii ambayo ina raha ya karaha. Hata mastaa nao iwe waimbaji, wacheza soka, waigizaji na wengineo wakitoka kwenye kazi zao ambazo zinawapatia mashabiki wengi, wanarejea makwao na kuishi maisha ya kawaida kama watu wengine. Wanashiriki kwenye shughuli za kijamii kama mwanadamu mwingine yoyote yule.

Nao pia wanafurahi, wanahuzunika na kuchukia pia. Ndiyo maana wanakereka, huwa wanatoa maneno ambayo baadhi ya watu wanawajia juu, bila kujua kuwa nao ni binadamu kama wao na ana nyongo pia. Ni lazima yakimfika shingoni awe na pa kuyatolea. Hata akifurahi pia anatakiwa aonyeshe furaha yake. Kwa sasa wanasanii wengi wanaonyesha hisia zao kwenye mitandao ya kijamii. Kwenye safu hii pia tutakuwa tukianika kile ambacho mastaa hao wanakitoa kwenye akaunti zao.

**GIGY MONEY**

Yeye kwenye akaunti yake ya instagram, msanii mwimbaji na mpamba video Gigy Money, katumia kujinadi na kujisifia. Raha jipe kwenyewe babu.

"Mungu ananipenda Namuomba, ndiyo mana nang'aa

Kote ni mimi 'natrendi', huku insta yani ndio balaa

Nang'aa kama simba. Simba baba lao nakimbiza makinda makinda watoto leo.

Wanaona natamba wanataka namba, matozi wanaoangwa, masnitch mapanga

Wanajitunisha wabei levo za Masaki, Obey, aaa hakuna chochote."

**RIYAMA ALLY**

Staa huyu wa bongo muvi, yeye akaonekana kukerwa na kutoa tahadhari kwa wazazi juu ya watoto zao huko Zanzibar, kwani baadhi huwa wanakwenda kucheza michezo ya hatari, ambayo ni kukimbia na kuruka juu, wakipinduka sarakasi na kutua ndani ya maji, au bahari. Akaweka video hiyo na kuandika hivi.

"Makachu Forodhani. Huu ni mchezi hatari sana kwa watoto wadogo. Mzazi ukipokea taarifa kuwa mtoto wako anashiriki huu mchezo tafadhari kuchukua tahadhari zote za kumzuia na kumkataza.

Siwezi kuwasemea watu wazima maana kila mtu ana starehe yake, Mungu awanusuru na mitihani."

Baadhi ya mashabiki wake alimjibu. Mmoja akaandika "Ni mchezo mbaya, ila unavutia kweli."

Mwingine akaaweka maandishi yake. "Kabisa, rafiki yangu alipoteza mtoto hapo hapo." Yupo aliyeandika hivi " Si mchezo kama mashindano ya kugelea tu dada?"

**SHAMSA FORD**

Msanii maarufu wa bongo muvi yeye hataki tabu kujiwekaweka kinyonge, akaandika.

"Furaha inakuja kwa kujitambua na kujiweka mbali na vitu vinavyokupa maumivu."

**AMBER LULU**

Huyu ni mwimbaji na mpamba video za muziki wa bongo muvi, yeye akaondoka maneno hafuatayo.

"Ni Bora uchafuke wakati wa kutafuta, kuliko kuwa omba omba msafi."

Dongo hili maana yake kuwa ni bora ufanye kazi yoyote ile ili upate mshahara mdogo halali, kuliko kuwa na pesa nyingi lakini ni za kuombaomba.

**NISHA BEBEE**

Huyu ni mwigizaji wa bongo muvi. Yeye anawajibu mashabiki wake ambao wamemisi sana kwenye uigizaji.

"Nilisimama kuigiza kwa miaka minne, ili 'nifokasi' na biashara tu. Haukuwa uamuzi rahisi, ilikuwa ni kama kuacha kitu unachokipenda huku hujui uendako kutakuwaje. Ila mmenifanya nisimame imara na niishi kwa sapoti yenu. Na hata kufanya yale wengi hawakutarajia wasanii tena wa bongo movie wanaweza fanya." Alindika kwenye instagram.



GIGY



## Dawa; Busara inaposhusha mihemuko

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine mtu hulazimika kufanya kitu ambacho kitatibu au kuzima kitu kingine ambacho kinamtesa na kumuumiza. Bila hivyo anaweza kupata tabu kwa muda mrefu au maisha yake yote. Pamoja na hayo busara inabidi itumike, kwako mwenyewe au kutafuta watu kwenye busara na si wenye mihemko.

'Dawa' ni filamu inayomhusu kijana Panama ambaye ametatizwa kwa muda mrefu kwenye ndoa yake. Anapata ushauri kwa watu mbalimbali. Wakamshauri mabaya na mazuri. Mwisho wa siku akaja kufanya jambo ambalo lilikua dawa ya matatizo yake.

Imechezwa na kina Madebe Lidai, Nusra Mbegu, Amini Ramadhani, Hussein Ramadhani, Aisha Bashiru, Zarina Hamisi, Shuku Kilwali, Mariam Hassan na wengine wengi

Panama anafanya kazi ya kubeba mizigo. Pesa anaipata kwa ugumu mno. Mkewe hajui hilo. Akitaka pesa anamfuata hadi kazini kwake. Na wakati mwingine anamchukua na kumkokota kwa nguvu kumrudisha nyumbani akiwa na 'maguo' yake ya kubebea mizigo.

Ni aibu kubwa, lakini mke wa Panama hajui hilo. Hali hiyo inawaumiza na kuwasononesha wenzake anaobeba nao mizigo.

Kuna siku anamwagiwa unga njiani, alipokutana ana mkewe, kisa alichelewa kumletea pesa ya kununulia unga, mpaka ikamlazimu kwenda kukopa.

Hali ikazidi kuwa mbaya, kina Madebe Lidai wakamuweka chini na kumwambia kwa matatizo anayoyapata inatakiwa 'akome' au akomae'.

Kobelo, mmoja wa marafiki wa Panama akatangaza kuwa mwezi ujao anaoa. Akazunguka kuwaarifu wote hadi nyumbani kwa Panama.

Siku ya harusi ikafika, mke wa Panama akavaa sare zake ambazo alizinunua kwa ajili ya harusi ya rafiki ya mumewe.

Alipofika nyumbani kwa Kombelo alichokiona kilimfanya ageuze njia. Kumbe muoaji hakuwa kobelo. Ni mumewe, tena akaoa binti mbichii. Kizunguzungu si kizunguzungu, presha si presha, hakumini kilichotokea.

Kumbe mchongo wote ule ulipangwa na Panama, pamoja na rafiki zake. Uamuzi ilikuwa ni kumuolea mke mwingine ili akili ikae sawa.

Na kweli, akili ikamkaa sawa. Pamoja na kurudi kwao, Panama alikwenda ukweni na kuwaambia wakwe zake kuwa wala hataki kumuacha mkewe.

Anataka wawe wawili ili wasaidiane baadhi ya mambo. Mkwe akamwambia binti yake arudi kwa mumewe kwa sababu kwa imani yao hajafanya kosa lolote.

Panama akawa na wake wawili, mke mkubwa akili ikamkaa sawa, heshima kwa mumewe ikarudi.



# Priyanka hivi Jonas kakutaliki?

MWIGIZAJI nyota wa filamu kutoka Bollywood, Priyanka Chopra, ameongeza joto la uvumi kwamba ameachana na mume wake Nick Jonas.

Uvumi kwamba ndoa ya wawili hao imesambaratika baada ya kuweka ujumbe katika ukurasa wake wa Instagram, ukionyesha hali si shwari.

Ujumbe huo unaosema "Hakika nimekufa katika mkono yako" ulionekana kuwashtua wengi na kuanza kujadili uhusiano huo kama umefika ukingoni.



## Pole Jessie kumpoteza mtoto

MWANAMUZIKI wa Uingereza, Jessie J, ametangaza kupoteza mtoto baada ya ujauzito wake kuharibika.

Nyota huyo wa muziki aliweka ujumbe katika ukurasa wake wa Instagram akisema anasikitika kuwa katika hali hiyo ya majonzi.

"Jana asubuhi nilikuwa nikicheka na rafiki yangu, ingawa nitapitia tamasha langu huko Los Angeles, bila kuwaambia watazamaji wote kuwa nina ujauzito". Ameandika.

## Kanye amtamani asali wake

BAADA ya kuishi maisha ya kulipiziana visasi, sasa rapa maarufu wa Marekani, Kanye West, anajaribu kufikiria kunusuru ndoa yake na Kim Kardashian, ambayo inafikia ukingoni.

Wanandoa hao ambao kwa sasa wametengana, kwa wiki kadhaa wamekuwa wakitunishiana misuli kwa kila mmoja kuonekana akiwa na mpenzi wake mpya, inaonekana kuwa Kanye anazidi kuteseka kiasi ambacho anaomba suluhu kati yao.

"Simulizi anazotaka Mungu ni kuona kwamba tunaweza kukombolewa katika mahusiano yote haya, tumefanya makosa, nimefanya makosa, nimefanya hadharani mambo ambayo hayakukubalika kama mume, lakini sasa hivi nataka kubadilisha simulizi," amesema.





## Mary waeleze, watakuelewa tu

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Mary Njoka, amesema wanawake wa kizazi cha sasa hawafanyi chaguo zuri la wanaume na kusababisha kuishi kwa tabu.

Akitoa maoni yake baada ya mwanamume mmoja kuelezea kisa chake cha kumrudisha mkewe nyumbani baada ya kushindwa kulala naye, Mary amesema ni lazima kuwapo na upendo katika uhusiano na si kulazimishwa.

"Nimeona kitu kimoja katika mtandao, mwanamke si chombo cha mapenzi, tunapenda mapenzi kwa kuhitaji furaha. Tusilazimishe kutokana na kulipwa hilo halitakiwi," amesema Mary.

## 2Face waonyeshe wewe ni mwanamume

MWANAMUZIKI maarufu wa Nigeria, 2face Adibia, amewataka watu kuacha kumshambulia mke wake Annie Idibia, kutokana na maoni yake kuhusu familia yake.

Akitumia akaunti yake ya Instagram, staa huyo aliwakabili wote wanaomsakama mke wake akisema ipo siku Mungu atawaadhibu.

"Mungu ataadhibu wote mnaomshambulia mke wangu kutokana tu na maoni yake," amesema?



# KWAHERI MZEE AL NOOR KASSUM

INATOKA UK. 7

• Aliwezesha wizara yake kufanya utafiti wa awali wa madini nchi nzima (kupitia airborne geophysical surveys) ambao matokeo yake, hatimaye, yalikuwa migodi mingi mikubwa na ya kati kuanzishwa mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000. Vilevile, utafiti huo ulisaidia katika juhudi za kutafuta na kuzalisha maji ya ardhini.

• Alihamasisha sana utafutaji wa mafuta na gesi. Kwa miaka mingi alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya TPDC na alishirikiana kwa karibu na Mkurugenzi Mtendaji wa shirika, Sylvester Barongo, pamoja na wataalamu wa shirika hilo wa fani za uwekezaji, usimamizi wa fedha, utawala, jiolojia na jiofizikia.

Wataalamu hao, ambao waliheshimika sana katika nchi za mashariki na kusini mwa Afrika ni pamoja na Yona Killagane, Salvator Ntomola, Halfani Halfani, Lionel Mawalla (marehemu), Yete Mwalyego (marehemu), Dismas Fuko, Herry Kejo Kajato, Joyce Singano na Flora Mpanju - kwa kuwataja wachache tu. Wengi wao walibobea kitaaluma kutokana na mikakati ya waziri wao ya kuendeleza rasilimali watu. Gesi ya Mnazi Bay iligunduliwa mwaka 1982 chini ya uongozi wake.

• Alifanya juhudi, kwa miaka 10 kuendeleza gesi ya Songo Songo ili itumike kwa ajili ya kutengeneza mbolea kwenye kiwanda cha Kilwa Ammonia Company (KILAMCO). Ingawa utekelezaji wa mradi wa mbolea ulishindikana na kuachwa mwaka 1989, jitihada za kuutekeleza ziliwapa watendaji wa Serikali uzoefu muhimu ambao ulisaidia kufanikisha utekelezaji wa miradi mbadala ya uzalishaji gesi kwa ajili ya kufua umeme na kuvipatia viwanda nishati.

• Aliishawishi serikali kuchukua mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa taasisi za fedha za kimataifa (Benki ya Dunia, Benki ya Rasilimali ya Ulaya na Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait) kwa ajili ya kuchoronga visima vya uendelezaji gesi kisiwani Songo Songo mwanzoni mwa miaka ya 1980.

Visima hivyo ndivyo vilivyowezesha uzalishaji wa gesi hiyo kibiashara kuanzia mwaka 2004. Benki ya Dunia ilikuwa haijawahi kuikopesha fedha nchi yenye pato la chini (kama Tanzania ilivyokuwa) kwa ajili ya uchorongaji wa visima vya utafutaji wa mafuta na gesi.




Al Noor Kassum (wa pili kushoto) na mkewe (wa pili kulia) wakiwa Ikulu jijini Dar es Salaam na Rais Mstaafu Jakaya Kikwete. Kulia ni waziri wa zamani, George Kahama na kushoto ni mkewe, Janeth Kahama. **PICHA: MAKTABA.**

• Alisimamia upanuaji wa gridi ya taifa ikaweza kufikia mikoa 15 na Zanzibar pamoja na uunganishaji wa Mkoa wa Kagera kwenye gridi ya Uganda. Alipoteuliwa kuwa Waziri anayeshughulikia nishati ni mikoa mitano tu iliyokuwa imeunganishwa kwenye gridi.

Upanuaji huo uliwashirikisha kwa kiwango kikubwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Salvatory Mosha (marehemu) na wasaidizi wake Simon Mhaville (marehemu), Baruany Elijah Luhanga, Silvanus Kimaryo (marehemu) na wengine wengi. Kwa kuijenga gridi ya taifa aliwezesha miradi ya gesi ya Songo Songo na Mnazi Bay kufanikiwa kibiashara kwa kupata soko kubwa la gesi ya kuzalisha umeme.

• Alisimamia maandalizi ya mradi wa umeme wa Stigler's Gorge ambayo yalihusisha usanifu kamili wa tuta, bwawa na kituo cha umeme pamoja na uchunguzi wa jiolojia na haidrolojia katika maeneo ya mradi pamoja na athari za kimazingira ambazo zingeweza kutokea wakati wa ujenzi na uendeshaji. Mradi haukutekelezwa kuanzia miaka ya 1990 kama alivyoshauri kutokana na gharama yake kubwa na ukosefu wa fedha. Hata hivyo, maandalizi aliyosimamia ndiyo yaliyotumika moja kwa moja na serikali kama msingi wa juhudi za miaka ya hivi karibuni za kuendeleza mradi huo.



Muonekano wa sehemu ya mradi wa umeme wa Julius Nyerere, wilayni Rufiji, ambao wazo la msingi lilitokana na Mzee Al Noor Kassum .

• Alianzisha mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya Nishati ya kwanza iliyotangazwa na serikali mwaka 1992. Prof. Matthew Luhanga wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (marehemu) na wataalam wengine walichangia kwa kiwango kikubwa katika maudhui ya sera hiyo.

Pamoja na mafanikio aliyoipatia Serikali akiwa kiongozi wa umma, Mzee Kassum aliweza kutunukiwa na Mtukufu Shah Karim al-Husayni, Mkuu wa Madhehebu ya Ismailia duniani, kuwa Vazir na mwakilishi wake nchini Tanzania. Aidha, baada ya kustaafu aliteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Morogoro.

Miaka michache iliyopita, Mzee Kassum alianza kudhoofika kiafya, hasa kutokana na umri wake mkubwa wa zaidi ya miaka 90. Septemba 2018 tulipata nafasi ya kumtembelea nyumbani kwake kumjulia hali na kumpa pole.

Mmoja wetu, Patrick Rutabanzibwa, alibahatika kumwona alipokuwa amelazwa katika Hospitali ya Aga Khan, Dar es Salaam siku nne kabla hajaaga dunia na kufikisha kwake salamu na shukrani za dhati kwa niaba ya watumishi wote aliowaongoza, kuwalea na kuwaendeleza katika kipindi chote alipokuwa kiongozi mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Mzee alikuwa amedhoofikakiasikwambahakuweza kuongea, lakini tabasamu yake iliashiria kuwa ujumbe ulifika.

**Pumzika kwa amani, Mzee Al Noor Kassum. Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu, na hakika Kwake tutarejea.**

***Patrick Rutabanzibwa amewahi kuwa Kamishna wa Nishati na Petroli, na Katibu Mkuu wa Wizara za Nishati na Madini; Maji na Umwagiliaji; Mambo ya Ndani ya Nchi; na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

****Prof. Mark Mwandosya amewahi kuwa Kamishna wa Nishati na Petroli, Katibu Mkuu wa Wizara za Maji, Nishati na Madini; Nishati na Madini; na Viwanda na Biashara. Amewahi pia kuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi; Maji na Umagiliaji; Maji; na Waziri wa Nchi (Mazingira), Ofisi ya Makamu wa Rais; na Waziri wa Nchi (Kazi Maalum), Ofisi ya Rais.**

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOELEKEA...

# Maisha ya sinema zama hizo na kumbi zilizotamba mijini

**Na Adam Fungamwango**



MIONGO kadhaa nyuma, kulikuwa na kumbi za sinema kila kona jijini Dar es Salaam na miji mingineo zilizotamba, hadi mwishoni mwa miaka ya 1990, wakati huo starehe hiyo ilikuwa kwenye chati.

Ni kwa sababu hakukuwa na televisheni, video, CD wala flash, hivyo ili kuangalia sinema ilikuwa ni lazima mtu atoke nyumbani, yeye peke yake au na familia yake aende sehemu maalum ambayo ilikuwa ikitumika kuonyesha filamu mbalimbali za mastaa ambao walivuma kipindi hicho.

Ukiwa sebuleni kwako, unaangalia filamu na watoto wake sasa hivi, halafu ukirudisha nyuma kumbukumbu kuwa zile picha ambazo unaziangalia leo sebuleni miaka ya nyuma ulilazimika kupanda basi kuzifuata, tena wakati mwingine kulanguliwa tiketi, au kufanya 'booking' wiki moja au mbili kabla, unabaki kucheka kimoyomoyo peke yake.

Unaweza ukadhani umekaa nchi mbili tofauti.

Tukianza na vijana waliozaliwa au kuishi Dar es Salaam wakati huo watakumbuka jinsi kulivyokuwa na kumbi mbalimbali za sinema zilizotamba

Watoto, vijana na hata watu wazima wa wakati huo, wakitaka burudani ya kuangalia filamu, wakati huo zikiitwa 'picha', ni lazima waende kwenye kumbi ambazo ni maalum kwa kuonyesha sinema mbalimbali za Kizungu, Kichina na Kihindi.

Kumbi zilizotamba jijini Dar es Salaam ni Cameo, Odeon, New Chox, Avalon, Emress, Empire, Star Light, bila kusahau Drive Inn Cinema.

Wenyewe watoto wa mjini waliuita 'Drai'. Huu ndiyo ukumbi maarufu zaidi wa sinema jijini Dar es Salaam kwa sababu haukuhitaji kuwa na kiingilio ili kwenda kutazama picha.

Ni uwezo wako wa kutembea tu kutoka unakoishi hadi hapo. Kwa vijana wa sasa, Drive Inn Cinema ni maeneo ya Msasani, ambapo kwa sasa kuna Ubalozi za Marekani.

'Drai' ilijengwa tofauti na kumbi zingine zote, nadhani nchini Tanzania kama siyo Afrika.

Wakati kumbi zingine zilijengwa kama majumba mengine ya starehe ambayo ni lazima ukate tiketi na kuingia ndani, 'Drai' ilijengwa kama vile uwanja wa mpira, tena vile vya mikoani, au Uwanja wa Uhuru. Na hata ukubwa wake unafanana na viwanja hivyo.

Lakini kulikuwa na ukuta mkubwa pembeni juu, kama vile jukwaa hivi ambalo lilitumika kuonyeshea sinema hizo. Wakati huo hata ukiwa maeneo ya Kinondoni, au Makumbusho na Kijitonyama, ukuta ule au 'bodi' la sinema, lilikuwa kinaonekana vizuri tu.

Kulikuwa na watu wa aina mbili waliokuwa wakitazama sinema maeneo ya Drive Inn.

Ulijengwa maalum kwa watu kwenda na magari na familia zao, ambapo walikuwa wakiingia ndani ya uwanja huo kupitia magetini na humo ndani kulikuwa na maeneo maalum ya kukaa watu na familia zao, pamoja na sehemu za kupaki magari yao. Na ndiyo maana ukaitwa 'Drive Inn'.

Aina nyingine ni wenzangu na mimi. Hawa nadhani ndiyo walikuwa wengi zaidi kuliko waliokuwa wanaingia na kulipa kwa pesa.

Walikuwa wakikaa nje ya uwanja au ukumbi huo, lakini walikuwa na uwezo wa kuangalia sinema vizuri tu. Tatizo lilikuwa moja. Watu waliokuwa nje ambao wote hakuwa wanalipa, yaani bure kabisa, walikuwa hawasikii sauti. Sauti ziliishia ndani kwa wale walioingia na magari yao.

Iliaminika kuwa waliokuwa wakiingia ndani mle na magari yao ni watu wenye uwezo tu, mabalozi, wakurugenzi, mameneja, wafanyabiashara wakubwa na watu wengine tu wenye pesa zao.

Sasa wale watoto wa vijana wa uswahilini, Kinondoni, Mwananyamala, Magomeni, Msasani, Mburahati, Kigogo, na wakati mwingine watu wazima, walikuwa wakijazana nje na kuangalia picha na ilikuwa kuanzia saa 12, wakati mwingine hadi saa nne usiku au tano.

Tabu nyingine ilikuwa ni mbu, kwa sababu ilikuwa nje na pembeni kulikuwa na majani mengi, kulikuwa na mbu wengi kiasi cha watu kusema 'Drai tiketi ni mbu,' wakiwa na maana sehemu ile haikuwa na kiingilio, lakini lazima uvumilie mbu.

Kuna baadhi ya watu ambao walikuwa wakiangalia sinema hizo kibubu-bubu nje ya 'Drai', lakini wakirejea nyumbani wanakuwa wasimuliaji wazuri na watafsiri kwa wenzao. Cha ajabu ni kwamba licha tu ya kutojua lugha ya Kiingereza au Kihindi, lakini hata sauti walikuwa hawasikii, lakini kwa kusimulia picha ilivyokuwa utadhani wao ndiyo watunzi wa huyo sinema.

Halafu kwa asilimia kubwa, watoto na vijana wa wakati huo walipendelea sana picha za kibabe.

Ni sehemu ambayo ilivuta wafanyabiashara wengi wa vyakula vidogo vidogo, kama 'ice cream', vinywaji na vitafunwa. Hata ule mtaa wa 'Maandazi Road' ulikuwa maarufu kwa sababu wengi walikwenda kununua maandazi maeneo hayo kwa ajili ya kutafuna wakati wanaangalia picha 'Drai'.

Mastaa waliokuwa wakitamba ni baba lao Bruce Lee, Angela Mao, Wang Yu, Sonny Chiba, Jim Kelly, Jackie Chan na wengine, huku kwa upande wa picha za kihindi kukiwa na Amitabh Bhachchan, Govinda, Mithun Chakraborty, Dharmendra, bila kumsahau Amrish Puri maarufu mama mzee Ashanti au Mugambo, kubwa la maadui.

Sinema zilizokuwa zikitamba wakati huo ni zile zote ambazo staa alikuwa Bruce Lee, War Bus, American Ninja, na nyingine nyingi, huku za kihindi ni 'Loha', 'Nasseb', 'Disco Dancer', 'Dance Dance', 'Andha Kanoon,'Hatya' na nyingine nyingi.


Kuna picha inaitwa Snake in the Monkey Shadow, iliyochezwa na Jackie Chan. Hii ilisababisha wengi kuiga staili yake ya kupigana mitaani ya kunyanyua mguu mmoja na mikono kuweka kama nyoka kobra anavyotaka kugonga mtu. Picha za Bruce Lee zilisababisha mtu akitaka kupigana avue shati.

Kumbi zingine ambazo zilikuwa zikionyesha picha hizo Sapna na Shaan zilizokuwa Morogoro, Metropole na Elite ambazo zilikuwa Arusha, huku Mwanza kulikuwa na kumbi kama Tovol Hall na Leberty Hall.

Mkoano Tanga, kumbi maarufu zilikuwa ni Majestic, Regal na Novelt, Geita wao walikuwa na ukumbi wa Mamlaka ya Pamba na Singida kulikuwa na Furaha Cinema.

**Kwa maoni tuma sms: 0716 350534.**



## Maandamano yazidi kushamiri Sudan

**Khartoom,** SUDAN

MAELFU ya watu wameingia katika mitaa ya Mji Mkuu wa Sudan, Khartoum na miji mingine wakiandamana kushinikiza viongozi wa kijeshi wa nchi hiyo kuachia mamlaka kwa utawala wa kiraia.

Katika mji wa Omdurman, vikosi vya usalama viliwarushia gesi ya kutoa machozi waandamanaji waliokuwa wakipinga mapinduzi ya mwezi uliopita.

Waandamanaji walikuwa wamekusanyika kutoa heshima za mwisho kwa makumi ya wenzao waliouawa na vikosi vya usalama vya Sudan katika wiki za hivi karibuni.

Waandamanaji hao pia walishutumu makubaliano ya hivi karibuni ya jeshi ambayo yalishuhudia Waziri Mkuu Abdalla Hamdok, akirejeshwa kwenye wadhifa wake.

Vyama vikubwa vya siasa na vuguvugu la waandamanaji wenye nguvu nchini Sudan wamepinga uamuzi wa Bw Hamdok kutia saini mkataba huo na jeshi.

Wengine wametaja kuwa ni usaliti au ni kuficha mapinduzi ya kijeshi kwa koti la kisiasa. **BBC**

## Ethiopia yaionya vikali Marekani

**ADIS ABABA** ETHIOPIA

SERIKALI ya Ethiopia imeionya Marekani kuacha kutangaza taarifa za uwongo kuhusu mapigano yanayoendelea na kutishia Mji Mkuu wa Addis Ababa.

Msemaji wa serikali Kebele Desisa, alisema vita vya Ethiopia havipambani tu na vikosi vya eneo la Tigray, bali pia mataifa ya Magharibi yenye nguvu.

Aidha ameitaka Marekani kusita kusambaza taarifa za uwongo zinazoikashifu nchi hiyo.

Kauli hiyo aliitoa kufuatia onyo la ubalozi wa Marekani, la kuwataka raia wake nchini humo kuondoka kwani kuna uwezekano wa kutokea shambulio la kigaidi.

Halikadhalika Marekani ilisema hakutakuwa na usaidizi kama ulitolewa wakati wa ghasia za Afghanistan iwapo mapigano yataingia Mji Mkuu wa Addis Ababa.

Baadhi ya Waethiopia walikasirishwa na matamshi hayo ya ubalozi wa Marekani, na kusababisha watu kuandamana nje ya ubalozi huo mjini Addis Ababa, wakipinga uingiliaji kati wa nchi za Magharibi katika mambo ya ndani ya nchi yao.

Majuzi Marekani imeonya kuwa hakuna suluhu ya kijeshi inayoweza kutuliza vita hivyo vya wenyewe kwa wenyewe, badala yake imeshauri kwamba mazungumzo ya kidiplomasia ndiyo njia pekee itakayoleta amani.

Taarifa hiyo ya Marekani ilitolewa muda mchache baada ya vyombo vya habari nchini Ethiopia kutangaza kwamba tayari yupo-uwanja wa vitakupigana-na-waasi/a-59927755" Waziri Mkuu Abiy Ahmed yupo uwanja wa vita ameungana na vikosi vyake vya kijeshi. **DW**

# Kirusi kipya cha corona chaibua hofu duniani

**GENEVA,** USWIZI

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limefanya mkutano maalum jana kujadili kuhusu aina mpya ya virusi vya Corona vinavyoenea kwa kasi nchini Afrika Kusini.

Wataalamu hao watakaa Geneva nchini Uswizi kuamua ikiwa kuna haja ya kuweka mkazo kuhusu wasiwasi wa virusi hivyo.

Ofisa Mkuu wa WHO alisema inaweza kuchukua mpaka wiki kubaini ikiwa idadi kubwa ya mabadiliko ya chembe za urithi za kirusi hicho ina athari kwa ufanisi wa chanjo zilizopo.

Hilo linakuja wakati Uingereza imeweka marufuku ya muda kwa safari zote za ndege kutoka Afrika Kusini na nchi tano jirani.

Wataalamu wa Afrika Kusini walisema kirusi hicho kipya kimeenea kwa kasi miongoni mwa wanafunzi mjini Pretoria.

Kirusi hicho kinaitwa B.1.1.529, huenda WHO likakipatia jina la Kigiriki kama lilivyo kwa kirusi cha Alpha na Delta.

Profesa Tulio de Oliveira, Mkurugenzi wa Kituo cha Kukabiliana na Magonjwa ya mlipuko nchini Afrika Kusini, alisema kulikuwa na mfululizo usio wa kawaida wa mabadiliko na kwamba kilikuwa tofauti sana na aina zingine za virusi ambavyo vimeenea.

Mwanasayansi mwingine Profesa Richard Lessells, kutoka Chuo Kikuu cha KwaZulu-Natal nchini humo, alionyesha wasiwasi virusi hivyo vinaweza kujiimarisha.

"Tunapata wasiwasi kwamba virusi hivi vinaweza kujiimarisha, na kuimarisha uwezo wake kuenea kutoka kwa mtu hadi mtu, lakini pia kinaweza kuepuka mfumo wa kinga." Alisema.

Hata hivyo, uchunguzi wa kisayansi katika maabara utatoa picha ya wazi, lakini majibu yatakuja haraka zaidi kutoka kwa ufuatiliaji wa mwenendo wa virusi duniani.

Bado ni mapema kutoa hitimisho la wazi kuhusu athari, lakini tayari kuna ishara ambazo zinaleta wasiwasi.

Kumekuwa na visa 77 vilivyothibitishwa katika jimbo la Gauteng, visa vinne nchini Botswana na kimoja Hong Kong.

Kuna matokeo ya haraka yanaweza kupatikana katika vipimo vya kawaida na ambayo inaweza kutumika kufuatilia kirusi hiki bila kufanya uchambuzi kamili wa maumbile.

Lakini hali hiyo haimaanishi kwamba kinaenea kwa kasi zaidi kuliko kirusi cha Delta, ni kikali zaidi au kwa kiwango gani inaweza kuepuka kinga inayotokana na chanjo.

Bado haijafahamika ni kwa kiasi gani tofauti kitaenea katika nchi zilizo na viwango vya juu zaidi vya chanjo kuliko asilimia 24 ya Afrika Kusini, ingawa idadi kubwa ya watu nchini humo wamekuwa na maambukizi ya Covid.

**BBC**



Wananchi wa Ethiopia wakiandamana kupinga mataifa ya nje kuingilia mapigano kati ya majeshi ya serikali na wanamgambo wa Tigray yaliyofanyika juzi mjini Addis Ababa. **(PICHA: BBC)**

# Watu 52 wafariki dunia baada mgodi kulipuka

**MOSCOW,** URUSI

WATU zaidi ya 52 wameripotiwa kufariki katika maafa mabaya zaidi kuwahi kutokea kwenye shughuli za uchimbaji madini nchini Urusi kwenye kipindi cha muongo mmoja uliopita.

Tukio hilo lilianza wakati vumbi la makaa ya mawe kwenye shimo la uingizaji hewa kushika moto Alhamisi, na kusababisha moshi mkubwa kwenye mgodi wa Siberia.

Kufikia usiku wa jana, operesheni iliyoshindwa ya kuwafikia wachimba migodi kadhaa waliotoweka iligeuka kuwa janga baada ya waokoaji kadhaa kuripotiwa kukosa hewa.

Wengi wa watu 285 katika mgodi wa Listvyazhnaya, katika eneo la Kemerovo kilomita 3,500 mashariki mwa mji mkuu wa Moscow, walikimbia baada ya tukio hilo.

Maofisa walisema majeruhi 49 wamefikishwa hospitalini kwa matibabu. Baadhi yao wana sumu ya moshi, na wanne wanasemekana kuwa katika hali mbaya.

Makumi ya wachimba migodi hawakuweza kukimbia baada ya tukio la awali, lakini shughuli za uokoaji zililazimika kusitishwa baada ya kiwango cha hatari cha methane kugunduliwa kwenye mgodi huo, na hivyo kusababisha hofu ya kutokea kwa milipuko.

Moja ya timu ya uokoaji ilishindwa kutoka mgodini. Miili ya waokoaji watatu ilipatikana baadaye, na kufanya idadi rasmi ya waliokufa kufikia 14.

Vyanzo kadhaa viliambia vyombo vya habari vya Urusi kwamba hakuna manusura zaidi waliotarajiwa kupatikana na idadi ya vifo imeongezeka hadi zaidi ya 50, wakiwamo waokoaji sita kwa jumla.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



Ndugu **REMIGIUS JOVIN MATUNGWA** (pichani) anatangaza kupotelewa na cheti chake cha shahada ya udaktari wa binadamu chenye namba KIUT0002248 kilichotolewa na Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala Tanzania mwaka 2020. Alisajilia chuoni hapo kwa namba **BMS/15098/501/DT.**

Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/555745/2021.**

Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0767352686.**

116580002

## KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI WA KAMPUNI YA **VASBAY LIMITED** YENYE NAMBA YA USAJILI **75360** WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA TAREHE **23th NOVEMBER 2021,** KAMPUNI YAO IMEFILISIKA NA HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI YA BRELA.

116589902

## KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI WA KAMPUNI YA **GNLT LIMITED** YENYE NAMBA YA USAJILI **133977** WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA **TAREHE 23th NOVEMBER 2021,** KAMPUNI YAO IMEFILISIKA NA HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI YA BRELA.

116589802

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No.172 Of 2021**

**In the matter of the estate of the late MARTIN COSMAS NGONDO of Chamwino District within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by MPOKI EDWIN MWAKAFUJE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 29/11/ 2021.

**Dated at Dodoma this 11/11/ 2021**

RESIDENT MAGISTRATE

116580602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GEOFREY RUTTA NYOMBI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyokuwa na namba ya usajili **T 832 CKV** Toyota Premio yenye chasis namba **AZT240-5005306** na engine namba **IAZ5000294 .** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/560440/2021**

116580702

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.146 OF 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE EZEKIEL CHIPASWA LUMBO of Veyula,**

**Makutopola Ward within City Council of Dodoma. AND IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY PAUL LUMBO CHIPWASA.**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 3 Day of 12, 2021

Dated at Dodoma this 12 Day of November,2021

116580902

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**LUDOVICK MANGWELA MWAJA .** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **FAIR DEAL AUTO PVT LTD** aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC 792 BQE.** Chassis No. **MD2A21BZ2HWK53274,** Engine No.**PF7WHL60246.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/520357/2021.**

116591002

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA MWANZA.**

**SHAURI LA MAOMBI NAMBA. 131 YA 2021.**

**SAMSON IBRAHIM.................. MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**KIHENGO MSOSO NA WENGINE WATATU.... WAJIBU MAOMBI**

**Kwa:** **1. KIHENGO MSOSO**
**2. MUGESI TEHATA**
**3. CHACHA MASIAGA**

**POPOTE WALIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Mfahamu kwamba, shauri tajwa hapo juu ambalo ninyi ni wajibu maombi limepangwa kusikilizwa mbele ya Mahakama hii tarehe 02.12.2021 saa 2:00 asubuhi

Hivyo mnatakiwa kuhudhuria Mahakamani ninyi wenyewe au wawakilishi wenu siku hiyo bila kukosa. Kutokuhudhuria kwenu kutaifanya Mahakama hii iendelee na shauri hili bila ninyi kuwepo.

Imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 11 mwezi NOVEMBA, 2021

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA.

116591202

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao walikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani nampenda kwa dhati. Alayempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-2

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Anapopita popote pale kila mmoja ni lazima amtazame mara mbilimbili. Labda kwa mtu ambaye hajamuona. Uzuri wale haukuwashangaza wanaume tu. Hata wanawake wenzake. Walishangaa kuona msichana na kibantu mwenye nywele ndefu kiasi kile, weupe, sura na pua kama ya kihindi.

Alikuwa kivutio vya wote. Na mwenyewe alilijua hilo. Ndiyo maana hakutaka kujiingiza kwenye mapenzi kirahisi kwa sababu alijua yeye ni kama ua. Kila nyuki analifuata. Lakini hakujua nyuki mwenye mapenzi halisi naye ni yupi. Hilo ndilo lilimtatiza.

"Hapa panatosha." Ilikuwa ni sauti yake, baada ya dakika mbili za ukimya.

"Okay mrembo, basi tutawasiliana, usisahau ahadi yetu."

"Hapana sisahau, ila ahsante sana."


"Usijali mrembo." Alisema Chala huku akiondoa gari taratibu, akizidi kuufaidi kwa macho uzuri wa Diana.

Chala alipagawa na msichana yule. Katika maisha yake alikuwa hajawahi kukutana na msichana ambaye amemfanya kusisimka na kushindwa hata maneno ya kuongea mbele yake kama yule.

"Huyu ndiye msichana ninayemhitaji. Huyu ndiye mwanamke wa maisha wangu. Nitafanya kila njia awe mikononi mwangu. Nimmiliki. Awe wangu. Awe mke wangu." Aliwaza mwenyewe akiwa njiani baada ya kugeuza gari yake kutoka Ubungo, akipita barabara na Sam Nujoma, kuelekea Kunduchi ambako anaishi.

Diana baada ya kuteremka, alikodi bodaboda kumpeleka nyumbani. Aliishi kwa mjomba wake, kaka wa marehemu mama yake Bishada. Angeweza kuishi peke yake kutokana na kazi anayoifanya. Lakini mjomba wake hakutaka aishi peke yake kwa sababu angeweza kuharibika na mambo ya mjini. Ingawa mwenyewe Diana alikuwa na nidhamu ya maisha, lakini alikubali kuishi kwa mjomba wake kutokana na kuepusha usumbufu kwa wanaume wanamfutilia.

Mjomba wake huyo ndiye aliyechukua hukumu la kumsomesha vema hadi vyuo kadhaa na kufanikiwa kupata kazi.




**Tinted ilikuwa ni moja ya hoteli za kisasa. Kwa upande wa mbele kulikuwa na mahema ya kisasa na watu walionekana kama wako nje hivi. Lakini wakiwa wamehifadhiwa kwenye mahema, yaliyopambwa na kunakshiwa marembo mbalimbali.**

Akiwa kwenye bodaboda alimuwaza Chala. Alianza kumjaji ni mwanaume wa aina gani? Anamfaa au? Alijua nia yake. Hakuwa mtoto kiasi hicho. Pamoja na kwamba amefuatwa na wanaume wengi. Amependwa na wanaume wengi, wametakiwa na wanume kibao. Lakini Chala ameonekana kumuweka sehemu tofauti. Siyo kwa sababu ana pesa au anamiliki kampuni. Ameshawahi kutakiwa na wanaume wenye pesa zaidi ya Chala na akakataa. Basi tu mwenyewe aliamua kumpa nafasi. "Awe mvumilivu tu, vinginevyo wakiwa mroho yatamshinda." alijisemea.

******************************

Kishindo kikubwa kilitokea. Gari dogo aina ya IST iligonga bodaboda na kuwafanya mwendeshaji na abiria wake kuanguka kwenye mtaro. Baada ya watu walikimbilia eneo la tukio kwa ajili ya kuwaibia waliopata ajali. Wengine wana roho nzuri, nia ni kuwasaidia. Lakini kama kawaida ya mijini. Kuna watu wao huona raha tu kukimbilia na kuangalia matukio mbalimbali, ikiwemo ajali.

Kwa bahati nzuri mwendesha bodaboda na abiria wake hawakuumia sana zaidi ya michubuko midogo midogo. Pamoja na hayo walitakiwa kwenda kwenye kituo cha polisi ili kupata PF3, itakayowawezesha kwenda hospitalini kufanya uchunguzi kuona kama watakuwa wameumia kwa ndani na matibabu.

Abiria huyo hakuwa mwingine ni Diana. Yule yule ambaye huwa anamchukua siku zote nyumbani na kumpeleka kituoni na kumchukua pia kituoni kumpeleka hadi nyumbani. Dereva aliyewagonga ndiye aliyelazimishwa kuchukua jukumu la kuwapakiza kwenye gari na kuwapeleka kwenye kituo cha polisi.

Mkuu wa kituo hicho alionekana kuvutiwa mno na uzuri wa msichana Diana.

"Naomba niachie namba yako, ili kama kutakuwa na taratibu zingine za kufuata, au chochote ambacho hakijakaa sawa, tuwasiliane."

Diana akatoa namba zake. Wakapata wanachohitaji na kwenda kwenye hospitali ya Amana kwa ajili ya matibabu.

Usiku wa saa nne, Diana akiwa amejipumzisha nyumbani alisikia simu yake inaita. Namba ilikuwa ngeni.

"Nani?"

"Mimi yule mkuu wa kituo pale Ubungo mlipokuja baada ya kupata ajali."

"Oooh, afande, nashukuru ahsante sana, nimeshatibiwa na niko vizuri, niko nyumbani kwa sasa nimepumzika."

"Okay, kama hutojali kesho unaweza kuwa na nafasi ukaja hapa kituoni?"

"Kwa masuala ya kikazi au?" Aliuliza Diana.

"Nusu kwa nusu." Alijibu, lakini Diana alihisi jambo. Mwenyewe alijifahamu. Ni Mrembo anayeweza kumtetemesha mwanaume yoyote hata akiwa mfalme achilia mbali afande.

"Kwa nini tusikutane sehemu nyingine nje ya kituo cha polisi, unajua mimi na mambo ya polisi ni tofauti, huwa muoga kweli, nakosa hata amani."

Afande alicheka na kumalizika na maneno haya "Huwa mnaogopa bure tu, polisi ni watu wema wenye kulinda raia na mali zao, ni rafiki wa wananchi, ila watu wabaya na wahalifu ndiyo mara nyingi wanaogopa polisi na hawa naonekana kama kuwaambukiza watu wengine ambao hawana matatizo yoyote kama wewe mrembo. Haya tukutane kesho saa moja usiku kwenye hoteli ya Tinted karibu na makutano ya barabara ya Shekilango na Morogoro."

"Okay, naifahamu hiyo afande nitakuja."

***************************************

"Naitwa afande Marco."

"Mimi naitwa Diana, nadhani jina langu unalijua kwa sababu jana uliliandika kwenye kitabi chako."

"Ni kweli."

Tinted ilikuwa ni moja ya hoteli za kisasa. Kwa upande wa mbele kulikuwa na mahema ya kisasa na watu walionekana kama wako nje hivi. Lakini wakiwa wamehifadhiwa kwenye mahema, yaliyopambwa na kunakshiwa marembo mbalimbali.

Watu wenye hela zao kwa sasa ndiyo wamekuwa wakikimbilia hapo kutumia. Ukiacha sehemu hiyo, kuna nyumba ya ghorofa moja ambayo ndiyo kuna vyumba vya hoteli hiyo. Chini ya sehemu ambayo watu wanapata vinywaji mbalimbali, na vyakula pia.

Hakuna yoyote kati ya afande Marco na Diana aliyeagiza bia. Kila mtu aliagiza soda.

Hata hivyo wote si kwamba hawanywi bia. Ni mazingira tu yamewafanya hivyo.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SERIKALI YAIBEBA TEMBO WARRIORS IKIIVAA MOROCCO

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya watu wenye ulemavu (Tembo Warriors), inatarajia kuwakabili wenzao kutoka Morocco katika mechi ya ufunguzi ya fainali ya mashindano ya Afrika (CANAF) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Katika kuiongezea hamasa timu hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan juzi aliwakabidhi Sh. milioni 150 ili ipeperushe vyema bendera ya Tanzania.**

Akizungumza kwa niaba ya Rais Samia, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema fedha hizo ni kwa ajili ya kusaidia maandalizi na mahitaji muhimu katika kipindi chote cha mashindano.

"Hizi fedha zimetolewa na Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, ni Sh. milioni 150, zifike kambini, zisimamiwe na zirati-biwe vizuri kwa ajili ya manufaa ya timu katika maandalizi na huduma zote za timu yetu ili kutuletea makombe,".

"Matumaini ya Rais wetu, Mhe. Samia Suluhu na sisi wasaidizi wake ni kuona Tembo Warriors mnafanya vizuri katika mashindano haya ambayo tumechukua uenyeji, basi tuingie uwanjani tukijua tunapeperusha bendera ya taifa huku Watanzania wote wanatuangalia, " alisema Majaliwa.

Aliongeza nafasi ya kuwa mwenyeji wa mashindano haya ni kubwa, lazima kama nchi tujivuni na tunatakiwa kuhakikisha mnapambana kutafuta ushindi kwa kila mechi.

"Kuanzia siku ya mashindano Watanzania watakuwapo hapa kwa sababu bendera ya taifa inapeperushwa huku wakiwa na imani ya ile kauli mbiu yetu, kwa Mkapa hatoki mtu, kwenu (Tembo Warriors), hiyo hivyo kutafuta ushindi kila mechi katika hatua ya makundi ili wapinzani wetu waingie uoga," Majaliwa aliongeza.

Naye Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Innocent Bashungwa alisema kwa kushirikiana na Chama cha Soka cha Watu wenye ulemavu Tanzania (TAFF), timu hiyo imeandaliwa vizuri na iko tayari kuipa nchi heshima.

"Nina imani na timu yetu ya Tembo Warriors itafanya vizuri kutokana na maandalizi iliyopata, tunatarajia Tanzania itakuwa miongoni mwa timu nne ambazo zitaenda kushiriki fainali za Kombe la Dunia mwakani," alisema Bashungwa.

Tanzania iliyoko Kundi A itashuka dimbani tena kesho kuvaana na Uganda na itamaliza mechi zake za hatua ya makundi keshokutwa Jumatatu kuvaana na Siera Lionne.

Fainali hizo zinashirikisha timu 14 ambazo ni pamoja na Kenya, Rwanda, Zanzibar, Liberia, Morocco, Uganda, Siera Lionne, Angola, Cameroon, Ethiopia, Ghana, Nigeria, Liberia na wenyeji Tanzania.

Fainali za dunia za michuano hiyo zimepangwa kufanyika mwakani nchini Uturuki.




Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Innocent Bashungwa ( wa pili kushoto) akizungumzia maandalizi ya fainali za soka za watu wenye ulemavu Afrika (CANAF), zinazofanyika nchini kuanzia leo. Kushoto ni Mchunguzi wa Lugha kutoka BAKITA, Ambrose Mganga, Katibu Mkuu wa TAFF, Moses Mabula na Kaimu Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Lwandamina kuendelea kuula Azam*

**Na Saada Akida**

HUKU timu yao ikiwa haina mwenendo mzuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Azam FC umeweka wazi hauna mpango wa kuachana na Kocha Mkuu, Mzambia George Lwandamina, imefahamika.

Azam FC imeweka wazi msimamo wake baada ya kuwapo kwa tetesi wanajipanga kuachana na Lwandamina na aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems anatajwa kurithi mikoba.

Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabiti 'Zaka Zakazi', alisema hakuna mchakato wowote uliofanywa wa kusitisha mkataba wa Lwandamina kwa sababu kocha huyo bado anaendelea na majukumu yake kama kawaida.

Zaka alisema bado uongozi una imani na kocha huyo licha ya kutokuwa na mwanzo mzuri kwenye msimu huu na matokeo mabaya waliyopata katika baadhi ya mechi ni ya kipindi cha mpito.

"Hatuna mpango wa kusitisha mkataba wa Lwandamina, kutoanza vizuri katika mechi zetu za ligi ni kipindi cha mpito, tuna imani na kocha tuliyekuwa naye na tutaendelea kuwepo hadi mkataba wake wa mwaka mmoja, utakapofikia tamati, " alisema Zaka.

Aliongeza wanaamini timu hiyo itaendelea kuimarika na kurejea kwenye makali yake na itafikia malengo iliyojiwekea katika msimu huu.

Azam FC itashuka tena dimbani Novemba 30, mwaka huu kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar kutoka mkoani Morogoro.

## Black Sailor FC yaipania Taifa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Black Sailor, Saleh Machupa, ametangazia 'vita' dhidi ya wapinzani wao Taifa Jang'ombe ambao watakutana katika mechi ya Ligi Kuu ya PBZ Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan.

Black Sailor yenye pointi 12 wako katika nafasi ya nne huku wapinzani wao Taifa Jang'ombe wana alama 14 na wako katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza visiwani hapa jana, Machupa alisema mchezo huo utakuwa mgumu kutokana na wapinzani wao kucheza kwa kutumia nguvu kubwa inayotokana na mashabiki wanaowafuatilia.

Machupa alisema hamasa wanayopata Taifa Jang'ombe inawasaidia wachezaji wake kupambana kutafuta ushindi katika kila mechi wanayocheza.

"Tumejipanga kuingia na mbinu ambayo wachezaji wangu hawatachanganyikiwa na mbinu ya hamasa inayotumiwa na wapinzani wetu," Machupa alisema.

## Friends of Namungo Liwale kimeeleweka

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Judith Nguli, ametoa Sh.350,000 kwa ajili ya ujenzi wa jiwe la msingi la ofisi ya Tawi la wanachama na mashabiki wa Namungo FC, liitwalo 'Friends of Namungo'.

Nguli alikabidhi fedha hizo juzi kwa Mwenyekiti wa tawi, Denis Mushi, katika hafla fupi iliyofanyika kwenye Uwanja wa Halmashauri ya Liwale kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa soka.

Kiongozi huyo alisema Namungo ndiyo timu kubwa iliyoko katika mkoa huko kwa sasa hivyo hana budi kuiunga mkono kwa hali na mali.

"Ninaamini tawi la Friends of Namungo litakalojengwa nje ya uwanja huu wa michezo litasaidia kuhamasisha wadau wa soka kuiunga mkono timu ya Namungo, lakini pia kuinua michezo wilayani mwetu," Nguli alisema.

Naye Mwenyekiti wa tawi hilo, Denis Mushi, aliwaomba wadau wa soka wa wilaya ya Liwale, kuacha kuzishabikia timu za Simba, Yanga na Azam FC, badala yake waiunge mkono Namungo FC ili iendelee kufanya vizuri zaidi kwenye Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE KUONDOKA PSG

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe (22), anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo wakati mkataba wake utakapomalizika msimu wa ujao. Newcastle United ni miongoni mwa klabu ambazo zinawaza kumwania mshindi huyo wa Kombe la Dunia.(Express)

### ZIYECH, WERNER HAO BARCA

WINGA wa Chelsea na Morocco, Hakim Ziyech (28) na mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, wanaonekana kama wachezaji mbadala wa winga wa Manchester City na England, Raheem Sterling mwenye miaka 26, wanaotarajiwa kujiunga na Barcelona Januari.(***ESPN***)

### POCHETTINO NA PSG

KLABU ya Manchester United haitamwajiri kocha wa PSG, Mauricio Pochettino, kwa sababu bodi haina mpango naye. (***Manchester Evening News***)

### STERLING NJIA MOJA

MANCHESTER City itapaswa kuongeza juhudi kumpa mkataba wa muda mrefu winga wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26 ambaye anahusishwa na Barcelona, ili aweze kusalia klabuni hapo. (***Telegraph***)

### VLAHOVIC SOKONI

MANCHESTER United imeungana na klabu nyingine, ikiwamo Tottenham Hotspur na Newcastle United, kutaka saini ya mshambuliaji Mserbia Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21 ambaye anaichezea Fiorentina. (***Mail***)

### ZIDANE, PSG WATETA

KLABU ya Paris St-Germain imefanya mazungumzo na Zinedine Zidane wakijiweka sawa na uwezekano wa kocha wao Mauricio Pochettino kuondoka na kujiunga na Manchester United. (***Le Parisien, via Metro)***

### RANGNICK RASMI UNITED

RALF Rangnick anatarajiwa kuwa kocha wa muda wa Manchester United, lakini awali alikataa ofa kutoka klabu hiyo ya Old Trafford kabla ya kukubali masharti mapya ya mkataba huo. (***Manchester Evening News)***

### POCHETTINO ATAJWA

MANCHESTER United bado inamtaka Mauricio Pochettino kuchukua mikoba ya ukocha klabuni hapo, licha ya kuwasili kwa Ralf Rangnick. (***90 Min***)

### SAVIC KUMRITHI POGBA

KIUNGO wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 26, anawaniwa na Manchester United kama mbadala wa Paul Pogba, ambaye mkataba wake na klabu hiyo ya Old Trafford unakwenda kumaliza mwishoni mwa msimu huu. (***Fichajes***)

### CABRAL ATAKIWA BARCA

BARCELONA wanafikiria kutupa ndoano kumsajili mshambuliaji wa Basel, Arthur Cabral lakini itabidi wauze baadhi ya wachezaji kabla ya kupeleka ofa kwa Mbrazil huyo mwenye miaka 23. (***Goal***)

### PERISIC HAJUI HATIMA

MKATABA wa winga wa Croatia, Ivan Perisic pale Inter Milan unakwisha Juni, 2022 na nyota huyo mwenye umri wa miaka 32 anasema "chochote kinawezekana, ngoja tuone wiki chache zijazo" alipoulizwa kuhusu mustakabali wake. (***Mediaset Infinity, via Football***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD : TUMPE HESHIMA SOLSKJAER

**Mshambuliaji huyo asema ni kocha ambaye United iko 'moyoni mwake'...**

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Marcus Rashford amesisitiza kocha wa zamani wa klabu hiyo, Ole Gunnar Solskjaer anastahili heshima, licha ya kufukuzwa pale Old Trafford.

United ilimfukuza Solskjaer baada ya kuchapwa mabao 4-1 kwenye Ligi Kuu England na Watford, kikiwa kipigo cha tano katika mechi saba za ligi hiyo msimu huu.

Solskjaer alianza kuwa kwenye wakati mgumu baada ya kutandikwa mabao 5-0 na Liverpool, huku pia wakichezea kichapo cha magoli 2-0 kutoka kwa majirani zao Manchester City kabla ya mapumziko ya kupisha mechi za kimataifa.

**Fowadi huyo wa zamani wa United, Solskjaer alichukua nafasi ya Jose Mourinho kama kocha wa muda Desemba, mwaka 2018 kabla ya kupewa mkataba wa miaka mitatu.**

Solskjaer aliiongoza United kumaliza nafasi ya sita mwaka huo na akamaliza nafasi ya tatu msimu wa 2019-20 na nafasi ya pili msimu wa 2020-21.

Hata hivyo, alishindwa kutwaa taji lolote, wakifika fainali mara moja na kufungwa na Villarreal kwa penalti kwenye Ligi ya Europa.

Na sasa Rashford amemtetea Solskjaer katika mahojiano na BBC akisema: "Ole yupo moyoni mwa Manchester United, hakuna anayepaswa kutomheshimu.

"Kwa upande wangu, anastahili heshima kubwa, sio kutoka kwetu tu, kutoka pia kwa mashabiki wote."

MECHI KALI
HOME
AWAY
TANZANIA PRISONS
2.51 | 2.51 | 3.29
NAMUNGO

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 710

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# CONTE: KIWANGO SPURS BADO

**LONDON,** England

ANTONIO Conte amebainisha "itachukua muda Tottenham kurudi kwenye kiwango chake" baada ya timu hiyo kufungwa mabao 2-1 na Mura kutoka Slovenia kwenye Ligi ya Europa Conference.

Harry Kane alionekana kuipa pointi Tottenham baada ya kusawazisha bao la Tommy Horvat pale kwenye dimba la Fazanerija, lakini Amadej Marosa alifunga goli la pili dakika ya mwisho kwenye mchezo huo, juzi Alhamisi.

Spurs ilifanya mabadiliko tisa kutoka kikosi kilichoshinda mabao 2-1 kwenye Ligi Kuu England dhidi ya Leeds United wikendi iliyopita na walicheza kwa muda mwingi wakiwa 10 baada ya Ryan Sessegnon kutolewa kwa kadi nyekundu.

Kipigo hicho kilikuwa cha kwanza kwa Tottenham chini ya Conte ambaye aliteuliwa mapema mwezi huu.

Conte, ambaye ana rekodi ya kushinda mechi mbili, sare moja na kipigo kimoja katika mechi zake nne tangu kuchukua mikoba ya Nuno Espirito Santo, amekubali kunahitajika mabadiliko makubwa.

"Hiki ni kipigo kibaya kwetu sisi. Kiwango kilikuwa kibaya," alisema kocha huyo wa zamani wa Inter Milan. "Tunajua tuna kazi kubwa ya kufanya mbele yetu. Huu ni wakati mgumu kwa upande wetu.



# Arteta amkaribisha Weng

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amemwalika, Arsene Wenger kurudi Arsenal akidai utakuwa "wakati mzuri kuwa naye jirani."

Wenger alichaguliwa kocha wa Arsenal mwaka 1996, akiwaongoza Washikabunduki hao kwenye mataji matatu ya Ligi Kuu England na saba ya Kombe la FA kabla ya kuondoka mwaka 2018.

Mfaransa huyo kwa sasa anafanya kazi kwenye Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), kama Mkuu wa Maendeleo ya Soka Duniani.

Arteta alicheza chini ya Wenger kwa miaka mitano kabla ya kustaafu mwaka 2016 na akachukua nafasi ya kocha msaidizi katika kikosi cha Manchester City, kabla ya kurithi mikoba ya kuinoa Arsenal hapo Desemba, mwaka 2019.

Baada ya kukutana hivi karibuni na Wenger mwenye umri wa miaka 72 katika uzinduzi wa filamu yake ya Wenger: Invincil teta alidokeza k anaweza kumka Wenger kurudi hapo.

"Kumekuwa r wasiliano, nil na nilizungumz wakati nilipo kuangalia filamu

"Kwa uhakika mtu wa aina y namkaribisha te rudi Arsenal," Arteta wakati gumza na waand habari."

## HABARI MICHEZO

# ,494,580

# JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.18 | 3.30 | 3.35 |
| 02. 27/11/21 | 18:00 | Hull City vs Millwall | 2.70 | 3.09 | 2.60 |
| 03. 27/11/21 | 18:00 | Huddersfield vs Middlesbrough | 2.46 | 3.10 | 2.85 |
| 04. 27/11/21 | 20:00 | Juventus vs Atalanta | 2.22 | 3.46 | 3.12 |
| 05. 27/11/21 | 20:30 | Mallorca vs Getafe | 2.43 | 2.90 | 3.30 |
| 06. 27/11/21 | 20:30 | Cercle Brugge vs Mechelen | 2.66 | 3.45 | 2.44 |
| 07. 27/11/21 | 20:45 | Fortuna Sittard vs Groningen | 2.72 | 3.26 | 2.47 |
| 08. 27/11/21 | 23:00 | Villarreal vs Barcelona | 2.69 | 3.33 | 2.57 |
| 09. 28/11/21 | 15:30 | Nurnberg vs St. Pauli | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 10. 28/11/21 | 17:00 | Brentford vs Everton | 2.38 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 28/11/21 | 17:00 | Bordeaux vs Brest | 2.42 | 3.34 | 2.84 |
| 12. 28/11/21 | 18:15 | Espanyol vs Real Sociedad | 3.30 | 3.25 | 2.22 |
| 13. 28/11/21 | 18:30 | Maritimo vs Pacos Ferreira | 2.66 | 3.10 | 2.66 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 27 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4018 | Kocaelispor vs Menemen Bld | 1.44 | 4.22 | 5.95 |
| 14:00 | 2208 | Ural Yekaterinburg vs Sochi | 4.52 | 3.49 | 1.75 |
| 15:00 | 1447 | FC Minaj vs Dynamo Kiev | 19.33 | 7.54 | 1.09 |
| 15:30 | 1728 | Preston vs Fulham | 4.02 | 3.58 | 1.81 |
| 15:30 | 2434 | Arsenal vs Newcastle | 1.53 | 4.34 | 5.66 |
| 16:00 | 3194 | Tanzania Prisons vs Namungo | 2.51 | 2.51 | 3.29 |
| 16:00 | 3676 | Alaves vs Celta Vigo | 2.90 | 3.10 | 2.55 |
| 16:00 | 4055 | Boluspor vs Eyupspor | 2.69 | 3.31 | 2.34 |
| 16:00 | 4290 | Mbeya City vs KMC | 1.75 | 2.98 | 5.19 |
| 17:00 | 1347 | Falkenbergs vs IK Brage | 3.44 | 3.69 | 2.01 |
| 17:00 | 1353 | Osters IF vs Akropolis IF | 2.46 | 3.30 | 2.85 |
| 17:00 | 2957 | Bryne vs Strommen | 1.44 | 4.52 | 5.39 |
| 17:00 | 3453 | Sampdoria vs Verona | 2.80 | 3.40 | 2.44 |
| 17:00 | 4737 | Empoli vs Fiorentina | 3.44 | 3.64 | 2.02 |
| 17:30 | 1002 | Greuther Furth vs Hoffenheim | 4.58 | 4.28 | 1.63 |
| 17:30 | 1464 | VfL Wolfsburg vs Borussia Dortmund | 2.83 | 3.43 | 2.38 |
| 17:30 | 1623 | FC Koln vs Monchengladbach | 2.78 | 3.63 | 2.33 |
| 17:30 | 3065 | Hertha BSC vs Augsburg | 2.10 | 3.23 | 3.58 |
| 17:30 | 5411 | VfL Bochum vs SC Freiburg | 3.14 | 3.34 | 2.24 |
| 18:00 | 1463 | Queens Park vs Kilmarnock | 3.19 | 3.48 | 2.00 |
| 18:00 | 1543 | Birmingham vs Blackpool | 2.11 | 3.23 | 3.38 |
| 18:00 | 2315 | Bournemouth vs Coventry | 1.87 | 3.38 | 4.01 |
| 18:00 | 3202 | Norwich City vs Wolverhampton | 3.50 | 3.25 | 2.15 |
| 18:00 | 3510 | Liverpool vs Southampton | 1.30 | 5.80 | 8.41 |
| 18:00 | 3729 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.18 | 3.30 | 3.35 |
| 18:00 | 3865 | St Johnstone vs Hibernian | 2.77 | 3.07 | 2.57 |
| 18:00 | 4161 | Dundee FC vs Motherwell | 2.37 | 3.30 | 2.86 |
| 18:00 | 4518 | Lothian Thistle vs Edinburgh City | 8.67 | 5.97 | 1.22 |
| 18:00 | 4632 | Ross County vs Dundee Utd | 2.70 | 3.19 | 2.55 |
| 18:00 | 5801 | Hull City vs Millwall | 2.56 | 3.05 | 2.76 |
| 18:00 | 5925 | Swansea vs Reading | 1.77 | 3.54 | 4.32 |
| 18:15 | 1996 | Asteras Tripolis vs Atromitos | 1.80 | 3.25 | 4.72 |
| 18:15 | 2987 | Valencia vs Rayo Vallecano | 1.99 | 3.36 | 3.86 |
| 19:00 | 1086 | Lille vs Nantes | 1.68 | 3.74 | 4.99 |
| 19:00 | 1976 | Samsunspor vs Adanaspor | 1.45 | 4.34 | 5.60 |
| 19:00 | 4169 | Besiktas vs Giresunspor | 1.53 | 4.13 | 5.51 |
| 19:00 | 4759 | FK Khimki vs FC Krasnodar | 4.33 | 3.59 | 1.75 |
| 20:00 | 2543 | Lillestrom vs Stromsgodset | 1.64 | 3.95 | 4.74 |
| 20:00 | 3815 | Juventus vs Atalanta | 2.23 | 3.45 | 3.11 |
| 20:00 | 5491 | Grasshoppers vs FC Lugano | 2.19 | 3.36 | 3.11 |
| 20:30 | 1707 | Bayern Munchen vs Arminia Bielefeld | 1.07 | 10.93 | 23.85 |
| 20:30 | 2153 | Brighton vs Leeds | 2.06 | 3.40 | 3.55 |
| 20:30 | 3041 | PAS Giannina vs AEK Athens | 4.24 | 3.45 | 1.82 |
| 20:30 | 3474 | Mallorca vs Getafe | 2.28 | 2.95 | 3.55 |
| 20:30 | 4796 | Apollon Smyrnis vs Lamia | 2.44 | 3.01 | 3.01 |
| 20:45 | 2188 | Fortuna Sittard vs Groningen | 2.84 | 3.28 | 2.37 |
| 22:30 | 5753 | FC Sion vs St. Gallen | 2.76 | 3.45 | 2.37 |
| 22:45 | 5614 | Venezia vs Inter | 7.22 | 4.91 | 1.39 |
| 23:00 | 2241 | Nice vs Metz | 1.41 | 4.68 | 6.97 |
| 23:00 | 3265 | Villarreal vs Barcelona | 2.63 | 3.31 | 2.64 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# RANGNICK ATUA RASMI OLD TRAFFORD



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa imemteua, Ralf Rangnick kuwa kocha wa muda wa timu hiyo.

Rangnick ambaye anatajwa kuwa ndio mwalimu wa makocha wa Ujerumani, akiwamo, Jurgen Klopp (Liverpool), Thomas Tuchel (Chelsea) na Julian Niglesmann, anatarajiwa kuchukua jukumu hilo kuanzia wiki ijayo.

Rangnick ambaye ana umri wa miaka 69 kwa sasa anaitumikia Lokomotiv Moscow kama Mkurugenzi wa Michezo na Maendeleo.

Msimu wa 2010/11 aliifikisha Schalke 04 hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya (walifungwa na Manchester United) na pia, walibeba Kombe la Ujerumani.

Rangnick pia aliiongoza RB Leipzig kwenye fainali ya mashindano ya Kombe la Ujerumani mwaka 2019.

Hatakuwapo kwenye benchi katika mchezo wa Jumapili ambao Manchester United itakabiliana na Chelsea, kwani anatarajiwa kukabidhiwa rasmi jukumu hili kuanzia Jumatatu.



# Chelsea yatangaza kumwania Araujo

**LONDON,** England

BEKI wa Barcelona, Ronald Araujo ameripotiwa kuingia kwenye rada za Chelsea ambapo wanataka kumsajili ili kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alijiunga na Barcelona akitokea klabu ya Boston River ya Uruguay mwaka 2018 na amecheza mechi 52 katika mashindano yote.

Araujo amekuwa mchezaji muhimu wa klabu yake kwenye msimu huu wa LaLiga, akiwa amecheza mechi 13.

Hata hivyo, majadiliano juu ya mkataba mpya hayaonekani kufikia hatua nzuri hadi sasa, na mkataba wa sasa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay hapo Camp Nou unatarajiwa kumalizika ifikapo Juni, mwaka 2023.

Kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo, klabu nyingi zinaendelea kufuatilia kwa ukaribu hali hiyo.

Ripoti hiyo inadai kuwa Chelsea inaonyesha nia ya kutaka kumsajili Araujo, huku Blues hao wakiamini ana sifa za kuwa imara katika soka la England.

ger

'Arsene ole', Ar- kwamba aribisha klabuni

na ma- imwona a naye kwenda yake. alikuwa ake na ena ku- alisema akizun- dishi wa

Michezo
Jumamosi Novemba 27, 2021
Nipashe



Rangnick atua rasmi Old Trafford UKURASA 23



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (katikati waliosimama), akiwa katika picha ya pamoja na wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors), ambayo inashiriki fainali za Afrika (CANAF), zitakazofanyika nchini kuanzia leo kwa kushirikisha mataifa 14. **PICHA: PMO**

# YANGA YAIHOFIA MBEYA KWANZA

## ●●● Yalazimika kupangua kikosi chake huku...

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikitarajiwa kuwasili jijini Mbeya leo tayari kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya wenyeji wao Mbeya Kwanza FC, vinara hao wamejipanga kucheza kwa 'tahadhari kubwa' huku wakiwafikiria watani zao, Simba, imefahamika.

**Mbeya Kwanza itaikaribisha Yanga Jumanne kwenye Uwanja wa CCM, Sokoine jijini humo huku vinara hao wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara wakitarajiwa kukutana na watani zao, Simba ifikapo Desemba 11, mwaka huu.**

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliliambia gazeti hili kikosi chao kimejipanga kuongeza umakini na nidhamu ili kupata ushindi katika mechi hiyo lakini pia wakipiga 'hesabu' za mchezo wao utakaofuata ambao watacheza dhidi ya Simba.

Bumbuli alisema wanataka kuona wanakuwa na wachezaji wao nyota kwenye mechi hiyo dhidi ya mabingwa watetezi ili wajihakikishie ushindi na si jambo lingine.

"Tutakuwa makini zaidi kwenye mechi yetu dhidi ya Mbeya Kwanza, tunajua mipango iliyopo, tutafanya hivi kujiweka katika nafasi salama kwa sababu tunahofia kupata kadi za njano na kupelekea baadhi ya nyota kuukosa mchezo dhidi ya Simba hapo Desemba 11, hili tumeshalifanyia kazi," alisema Bumbuli.

Kiongozi huyo alisema kikosi chao kimejiandaa vizuri na kiko tayari kuvuna pointi tatu muhimu katika mchezo huo wa raundi ya saba.

"Msafara wetu utakuwa na nyota 22 na tunatarajia kuondoka Dar es Salaam kuelekea Mbeya siku ya Jumapili (kesho), kwa ajili ya mchezo dhidi ya Mbeya Kwanza, tunajua ni timu ambayo imejipanga pia na imeanza msimu vizuri," Bumbuli alisema.

Aliongeza wanatambua umuhimu wa mchezo huo na akaweka wazi huenda baadhi ya wachezaji wao tegemeo wakaukosa mchezo huo kwa sababu mbalimbali.

"Tumebaini janja janja za wapinzani wetu kuwatafutia kadi za njano wachezaji wetu nyota, au kufanyiwa rafu za makusudi akiwamo, Khalid Aucho na wengine ili kushindwa kucheza mechi ijayo dhidi ya Simba,"

"Tumegundua na tunatarajia mechi yetu dhidi ya Mbeya Kwanza itakuwa na mabadiliko katika kikosi, baadhi ya nyota watapumzishwa kwa ajili ya kujiandaa na pambano letu dhidi ya Simba, tunawahakikishia mashabiki wetu tutarejea na pointi tatu kutoka kwa Mbeya Kwanza halafu Desemba 11, tabu iko pale pale dhidi ya Simba," alisema Bumbuli.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, aliliambia gazeti hili wachezaji wote wako katika hali nzuri kuelekea mchezo huo na wamejiandaa kucheza kwenye uwanja ambao sio rafiki.

"Tumepata siku za kutosha kurekebisha mapungufu yote ambayo yalitupa changamoto, lakini pia wapo wachezaji ambao tuliwakosa kutokana na maumivu na wakati huu tutakuwa nao," alisema Nabi.

Wakati huo huo Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa Mbeya City kuwakaribisha KMC FC wakati Namungo FC itawafuata 'Maafande' wa Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela ulioko Sumbawanga mkoani Rukwa.

Mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba ambao ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wao watashuka dimbani Desemba 1, mwaka huu kuwakaribisha Geita Gold kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

# Serikali: Twendeni tukaishangilie Simba

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Innocent Bashungwa, amewaomba Watanzania na wadau wa soka kuonyesha ushirikiano wakati timu za Taifa na klabu za hapa nchini zinapokuwa zinapeperusha bendera ya nchi katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ili kuzipa hamasa.

Bashungwa ametoa kauli hiyo baada ya kuwatakia kheri Simba ambao kesho wanashuka dimbani kuwavaa Red Arrows ya Zambia katika mechi ya kwanza ya hatua ya mtoano ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Bashungwa alisema Watanzania wanatakiwa kuweka pembeni ushabiki wa timu zao pendwa inapofika wakati mpinzani wake anaiwakilisha nchi katika michuano ya kimataifa.

Bashungwa alisema serikali inaiombea Simba ipate ushindi katika mchezo wao dhidi ya Red Arrows kwa sababu matokeo hayo yana umuhimu kwa maendeleo ya soka nchini.

"Tuondoe ushabiki wetu na kusapoti timu zetu zinapowakilisha nchi, umoja tulionyesha kwa timu zetu za Taifa ikiwamo Taifa Stars basi umoja huo uonyeshwe katika klabu zetu zinapowakilisha Taifa, tusiwabeze na kuwapa kipaumbele wapinzani," alisema Bashungwa.

Aliongeza Simba ikifanya vizuri na kusonga mbele katika michuano hiyo ya kimataifa, itakuwa imelipa taifa faida kwa sababu itaongeze pointi zitakazowezesha kupata fursa ya kuingiza nne kama ilivyokuwa kwenye msimu unaoendelea.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >